# Nipashe

Jumamosi Mei 16, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580233

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Watu saba wafa maji, wanne wa familia moja

UKURASA 3




UKURASA 11

# Wabunge Chadema watinga bungeni

**SPIKA** asema hawakufukuzwa walitakiwa warudishe fedha walizochukua...*Endelea ukurasa 2*



Wafanyakazi wa Bandari ya Mwanza Kusini, wakiendelea kushusha tani 20,000 za sukari na kuzipakia kwenye magari ili kusambazwa mikoa mbalimbali, baada ya kuwasili na meli bandarini hapo juzi, kutoka nchini Uganda. **PICHA: ELIUD RWECHUNGURA**

## Watanzania 246 waliokwama India warejea

UKURASA 2

## WAGONJWA 42 WA CORONA WALAZWA VITUO VITATU

UKURASA 2

## BAA LA CORONA



Katika kipindi hiki cha mlipuko wa ugonjwa wa Covid-19, unashauriwa kuwa na mawasiliano na watu uwapendao na unaowaamini kila siku au kadiri unavyoweza kwa kutumia simu, video au kutuma ujumbe mfupi. Tumia muda huu kuwaeleza unavyojisikia na kuwashirikisha vitu unavyopenda kufanya nao pamoja. WHO

- **Epuka mikusanyiko ya watu**
- **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
- **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
- **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



MICHEZO **TFF MATATANI FEDHA ZA JPM** UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# Wabunge Chadema watinga bungeni

**Na Waandishi Wetu**

WABUNGE watano wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) waliokuwa kwenye eneo la kujitenga kwa maelekezo ya chama chao, jana walitinga bungeni kuendelea na vikao.

Wabunge hao walikuwa hawajahudhuria vikao wala kufika eneo la Bunge tangu Mei mosi, mwaka huu, baada ya chama hicho kuwataka kujitenga kwa ajili ya kufuatilia afya zao ikiwa ni namna ya kukabiliana na virusi vya corona.

Waliohudhuria vikao kwa siku ya jana ni Ester Matiko (Bunda Mjini), Frank Mwakajoka (Tunduma), Salome Makamba (Viti Maalum) na Devotha Minja (Viti Maalum).

Mbunge Aida Khenan yeye alionekana katika viwanja vya Bunge.

**SPIKA AFUNGUKA**

Jana wakati wa kuhitimisha kikao cha Bunge, Spika Ndugai alisema hakuna mbunge yeyote aliyefukuzwa bungeni, bali walijifukuza wenyewe.

Alisema tatizo kubwa ni wabunge hao (upinzani) kuchukua fedha na 'kuingia mitini'.

"Kuna baadhi ya wabunge wa upinzani wamekuwa wakiropoka katika mitandao ya kijamii akiwamo Mbunge Rhoda Kunchela (Viti Maalum, Rukwa), akimtuhumu Mbunge wa Musoma Vijijini, Nimrod Mkono, kuwa mbona amepokea fedha za 'Per diem' lakini hajahudhuria Bunge, eti kwa sababu ni wa CCM," alisema Ndugai na kuongeza:

"Mzee Mkono atalipwaje fedha wakati hajawahi kuhudhuria kikao hata kimoja, Mkono anaumwa sana tena sana na anahitaji maombi yetu, hajitambui, leo binti mdogo kama wewe unamtuhumu mtu ambaye ni baba yako eti kachukua fedha," alisema Ndugai.

Kutokana na hali hiyo, Spika Ndugai alimtaka Mbunge Kunchela kuomba radhi ama kuthibitisha maneno hayo aliyoyatoa.

Spika Ndugai alisema tabia ya kuropoka hasa kwa wabunge siyo nzuri na kwamba kuwa mbunge wa upinzani kisiwe kigezo cha kuropoka.

**AGIZO LA CHADEMA**

Baada ya wabunge kutii agizo la chama lililotolewa na kusainiwa na Mwenyekiti wa Chadema Taifa, Freeman Mbowe, Spika aliwataka kurejea bungeni haraka iwezekanavyo.

Wabunge 11 wa chama hicho hawakutii maelekezo ya chama hicho na kuendelea kuingia bungeni, siku chache baadaye, Kamati Kuu ya chama hicho iliazimia kuwachukulia hatua za kinidhamu kwa kuwafukuza wanne, kumvua nyadhifa zote za ndani ya chama mmoja na wengine tisa kutakiwa kujieleza kwanini wasichukuliwe hatua.

Spika aliwataka wabunge hao kurejesha fedha Sh. milioni 110.1 walizolipwa kwa ajili ya kujikimu, huku akitaka kila mmoja, kurejea bungeni akiwa na majibu ya vipimo vya corona vikionyesha hawana maambukizo.

Pia alisema iwapo hawatatimiza masharti hayo mishahara yao ya mwezi Mei, itakuwa hatarini na kwamba anawasiliana na mamlaka mbalimbali ili kuangalia namna ya kulishughulikia suala hilo.

Wabunge waliofukuzwa na chama chao na wameendelea kuhudhuria vikao vya bunge ni David Silinde (Momba), Wilfred Lwakatare (Bukoba Mjini), Joseph Selasini (Rombo) na Antony Komu (Moshi Vijijini).

**CHADEMA YANENA**

Jana, Chadema kilitoa taarifa kwa umma kuwa wabunge wake wamehitimisha siku 14 za kujitenga na walianza kurejea bungeni kuendelea na vikao vya Bunge.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano Chadema, Tumaini Makene, wabunge hao walikuwa wamejitenga kwa kukaa ndani na kutohudhuria shughuli za Bunge, vikiwamo vikao vinavyoendelea bungeni.

Alisema wabunge waliotekeleza uamuzi wa makubaliano ya chama ya kujitenga kwa kutofika maeneo yote ya Bunge walitekeleza masharti na ushauri unaotolewa na wataalamu wa afya namna bora ya kujitenga na kupunguza maambukizo.

"Wabunge wetu wote walitekeleza makubaliano na uamuzi wa chama na wabunge wa kujitenga kwa siku 14, ambayo yanatokana na maelekezo na ushauri wa wataalamu wa afya ikiwamo Shirika la Afya Duniani (WHO),"alisema.

Mnyika alisema msingi wa makubaliano hayo umetokana na maelekezo na ushauri wa WHO ambayo yamethibitisha kuwa kujitenga ni moja ya njia zilizothibitishwa kisayansi katika kuzuia na kupunguza maambukizo ya corona.

***Imeandikwa na Gwamaka Alipipi (Dodoma) na Romana Mallya***

## Wagonjwa 42 wa corona walazwa katika vituo 3

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imesema kuwa hadi juzi kulikuwa na jumla ya wagonjwa 42 waliolazwa katika vituo vitatu vya wagonjwa wa corona jijini Dar es Salaam na Pwani.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Profesa Mabula Mchembe, alisema hayo wakati wa makabidhiano ya vifaa kinga kutoka kwa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, jijini Dar es Salaam.

Alisema hadi juzi wagonjwa wanaoendelea na matibabu katika vituo hivyo na idadi yake kwenye mabano ni Hospitali ya Amana (12), Kisoka Mloganzila (6) na Kibaha (24).

Alisema wengi wa wagonjwa katika vituo hivyo wanaendelea vizuri, na kwamba ni vyema watoa huduma za afya kuwahudumia wagonjwa wote wanaofika katika vituo vya afya bila ubaguzi.

"Ninawaasa watoa huduma za afya kuwahudumia wagonjwa wote wanaofika katika vituo vya afya, bila ubaguzi kwa kuwa wapo wagonjwa wengine hawaumwi corona bali wanayo magonjwa mengine ambayo yanahitaji huduma za matibabu ya kila siku," alisisitiza Profesa Mchembe.

Vile vile, alizishukuru hospitali binafsi kwa ushirikiano katika kuwahudumia wagonjwa wa corona na wagonjwa wengine na kwamba hilo linaleta matumaini katika mapambano ya janga hilo.

Kwa upande wake Balozi wa China nchini, Wang Ke, alisema kama ndugu wa karibu baina ya nchi hizo mbili wameamua kukabidhi vifaa hivyo kwa ajili ya watoa huduma za afya, kukabiliana na ugonjwa huo ili kusaidia kuwalinda watoa huduma katika sekta hiyo.

Serikali ya China ilitoka msaada wa vifaa kinga vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 700, makabidhiano ambayo yalifanyika kwenye Bohari Kuu ya Dawa (MSD).

Baadhi ya vifaa vilivyokabidhiwa ni barakoa aina ya N95, barakoa za upasuaji, glavu, buti, nguo za kujikinga, miwani ya kulinda macho na vipima joto.

# Watanzania 246 waliokwama India warejea

**Na Beatrice Moses**

WATANZANIA 246 waliokwama India kutokana na kizuizi (lockdown) kilichowekwa kudhibiti maambukizo ya virusi vya homa kali ya mapafu Covid-19 wamerejea nchini na kudai kuwaacha wengine kutokana na kushindwa kulipa nauli ya Dola za Marekani 850.

Waliowasili miongoni mwao ni wagonjwa, wanafunzi na wafanyabiashara, ambao waliingia jana saa 4 asubuhi baada ya serikali kutuma ndege ya Shirika la Ndege Tanzania (ATCL).

Mmoja wa wanafunzi waliorejea alieleza kuwa kuna wenzao wamebaki nchini India, akidai kushindwa kumudu kulipa gharama za nauli na kuishauri serikali kupunguza kiwango cha gharama hizo na kuandaa utaratibu wa kuwafuata.

"Serikali iwaangalie wale waliobaki kule iwapunguzie kiwango cha nauli, Dola 850 kwa wengine inaweza kuwa siyo nyingi, lakini kwa wengine ni changamoto," alisema.

Mathias Kitambi, alisema kuwa wamekumbana na changamoto kadhaa kutokana na kizuizi kichowekwa nchini humo, ikiwa ni pamoja na kulazimika kula vyakula vya aina moja, kwa muda mrefu.

Alisema kuwa waliwekwa karantini, kwenye hosteli moja ya vyuo vya huko na kula wali na mchuzi, tofauti na wenzao waliokuwa nje ya hapo waliomudu kuagiza vyakula tofauti.

"Tumesafiri umbali mrefu kwa mabasi ndani ya muda wa siku tatu kwenda Mumbai ili kupanda ndege, mimi nipo mwaka wa tatu, tulikuwa tunaendelea na masomo kwa online, uongozi wa vyuo umesema tunaweza kufanya mtihani wetu wa kumaliza kwa njia ya online," alisema.

Alisema, hali ya uchumi ilianza kuyumba hasa kwa wageni na baadhi hawajafanikiwa kurudi, mahitaji muhimu ilikuwa ni magumu, pia hata usafiri wa ndani kutoka eneo moja kwenda lingine umezuiliwa.

Kalvin Christian ambaye ni mwanafunzi alieleza furaha yake ya kufanikiwa kuwasili nchini, akiishukuru serikali kuwaongoza vyema tangu wakiwa India hadi walipotua nchini Tanzania.

"Tumewaacha wanafunzi wenzetu wengine kwa sababu mbalimbali, nafikiri pia kulikuwa na mchakato mkubwa wa kufuata ili kufanikiwa kutoka India," alisema Christian.

Suleiman Harid, aliishukuru serikali kwa kutuma ndege kwenda kuwafuata, akibainisha kuwa imeonyesha jinsi inavyowajali.

Alisema kwamba wakiwa India walichukuliwa vipimo upya vya corona, na walikuwa wamefungiwa bila kutoka, walipofika nchini pia wamechukuliwa vipimo ikiwamo kupimwa kiwango cha joto.

Wiki iliyopita, Msemaji wa Serikali, Dk. Hassan Abbas, alisema serikali itatuma ndege kwenda kuwachukua wananchi hao Mei 11, kuelekea India na itarejea nchini Mei 12.

Dk. Abbas ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, alisema kuwa hatua hiyo itafuatia kutokana na mawasiliano ya muda mrefu baina ya watu hao na serikali, ambayo ilikamilisha taratibu zote zilizohitajika ikiwamo kuomba vibali vya kurusha ndege na kutua India hasa katika kipindi hiki ambacho kumekuwa na vizuizi kutokana na corona.

JOSINA COMPANY LIMITED & AUCTIONEER.
DALALI WA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA – MKOA WA MWANZA
DEBT COLLECTIONS & AUCTIONEERING
HEAD OFFICE –Buzuruga plaza 2nd Floor Room No. 207 Mwanza
P.O BOX 11126 MWANZA, 0713/0789/0768-203040
josinacompany@gmail.com,josinacoltd@gmail.com

TANGAZO TANGAZO TANGAZO

KWA AMRI TULIYOPEWA NA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA, MKOA WA MWANZA. JOSINA COMPANY LIMITED WATAENDESHA MNADA WA HADHARA WA KUUZA VIWANJA VINNE(4) VYENYE JUMLA YA UKUBWA WA 37,400M2 .PLOT NAMBA 1,2,3,4 BLOCK (A) ILUNGU AREA, WILAYA YA MAGU. ENEO LIMEPAKANA NA NYANZA COTTON INDUSTRIAL.VILIVYOKUWA VINASHIKILIWA NA WAKWEPA KODI NDG-VISHAL SODHA. NI ENEO LA VIWANDA NA LIKO BARABARA KUU YA MWANZA-MUSOMA.MNADA UTAFANYIKA TAREHE 22/05/2020.

AMRI HII INATOKANA NA SHAURI LA MADAI NAMBA 114 YA 2019 KATI YA KAMISHINA WA ARDHI- MWANZA NA VISHAL SODHA WA MWANZA.

MASHARTI YA MNADA:
1. VIWANJA HIVI VITAUZWA KAMA ZILIVYO, MNUNUZI ATALIPIA 25% YA BEI YA MNADA. NA 75% ITALIPWA NDANI YA SIKU 14 KUTOKA SIKU YA MNADA. AKISHINDWA KULIPA, MALIPO YA AWALI HAYATARUDISHWA.
2. UKAGUZI WA DHAMANA ZINAZOUZWA UTAANZA LEO SIKU YA 13/05/2020 KABLA YA MNADA NA GHARAMA ZA KUMPELEKA MTEJA KWENYE DHAMANA ZITAKUWA JUU YA MTEJA.

KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA:-
MKURUGENZI
Josina Co. Ltd: 0768 203 040,
WHATSAPP NO: 0713 203 040.
XXXXX

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

Tarehe 16-05-2020

TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **Jumatatu tarehe 18-05-2020** kampuni ya **ESTIM CONSTRUCTION CO. LTD** itasafirisha Mzigo Motor Grader wenye vipimo vikubwa kutoka **Kiwangwa kuelekea Dar es salaam** kupitia Msata na Vigwaza. Gari hilo lenye namba za usajili: **T 595 AZB / T 106 AYZ**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   Urefu - mita 20.00
   Upana - mita 3.0
   Kimo - mita 4.8
3. Njia itakayotumika: Kiwangwa hadi Dar es salaam kupitia Msata na Vigwaza. Magari yatasafiri muda wa mchana tu **(kuanzia saa 12:30** Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**
157431

## HABARI KITAIFA



Mkuu wa Wilaya ya Bahi, mkoani Dodoma, Mwanahamisi Mkunda (kulia), akikagua sehemu ya mpunga uliookolewa na wakulima kutoka kwenye maji, alipotembelea kukagua mashamba ya zao hilo, yaliyofunikwa na maji ya mvua zinazoendelea kunyesha katika mikoa ya jirani, zaidi ya hekari 11,000 zimeathirika. **PICHA PAUL MABEJA**

# Saba wafa maji, wanne familia moja

**Na Waandishi Wetu**

WATU saba wamekufa maji, wanne wa familia moja katika matukio mawili tofauti mjini Bagamoyo, mkoani Pwani na Bunda mkoani Mara.

Tukio la vifo vya watu wanne wa familia moja limetokea Kitongoji cha Amani, Kata ya Kerege, Wilaya ya Bagamoyo, baada ya watu hao kuzama katika dimbwi la Mto Mkuza.

Kamanda wa Polisi, mkoani Pwani, Wankyo Nyigesa alithibitisha kutokea kwa tukio hilo Mei 14, majira ya saa 11 jioni katika kitongoji hicho.

Aliwataja waliokufa kuwa ni Juma Charles (21), Emmanuel Charles (21), Felister Charles (18) na Ashura Emmanuel (23), wote wakazi wa Amani.

Chanzo cha tukio hilo inadaiwa kuwa wote walikuwa wakivua samaki katika mto huo na mmoja wao alizama na katika jitihada za kumuokoa, wengine waliingia na kunasa kwenye tope na hivyo kushindwa kujiokoa.

Kamanda Wankyo aliwatahadharisha wananchi kuwa makini wanapofanya shughuli zao karibu na madimbwi na mito hususani katika kipindi hiki cha mvua kwa kuwa ni hatari kwa maisha yao.

Tukio lingine limetokea wilayani Bunda mkoani Mara, wakati watu watatu wakazi wa kijiji cha Tamau, Kata ya Nyatwali, kufa maji katika Ziwa Victoria, baada ya mtumbwi wao kugongana na mtumbwi wa wavuvi haramu ambao walikuwa wameiba nyavu zao.

Wakizungumza na Nipashe jana kwa nyakati tofauti katika eneo la Mwalo wa Nyatwali, Mwenyekiti wa Mtaa wa Tamau, Asaph Ernest na Ofisa Mtendaji wa Kata ya Nyatwali, Dainos Sijaona, walisema tukio hilo lilitokea Mei 11, mwaka huu majira ya alfajiri, baada ya wavuvi hao kwenda kufuatilia nyavu zao.

Walisema baada ya kufika katika eneo hilo na kuziona nyavu zao waliwasiliana na ndugu zao waliokuwa nchi kavu kwa njia ya simu, lakini ghafla mawasiliano hayo yalikatika na hawakupatikana tena.

"Waliondoka siku hiyo majira ya alfajiri baadaye wakawasiliana na ndugu yao kwamba nyavu zao wameziona na kusema kwamba watatutaarifu baadaye, lakini ghafla mawasiliano yakakatika na ndipo tukaamua kuwafuatilia na kukuta mtumbwi upo majini ukiwa umezama bila wao kuwamo," alisema Asaph Ernest, Mwenyekiti wa Mtaa wa Tamau.

Wenyeviti wa mitaa ya Yowe na Tamau, walisema kuwa baada ya mawasiliano kukatika wananchi waliwafuatilia na kukuta mtumbwi na kufanikiwa kupata miili ya watu wawili na mmoja ulipatikana baada ya siku tatu.

"Nilipigiwa simu na mwenyekiti wa mtaa kuhusu tukio hilo, wananchi wakaanza kufuatilia na kufanikiwa kupata miili ya wavuvi wawili, lakini tunashukuru Mungu mwili wa mvuvi mmoja umepatikana leo (jana)," alisema Sijaona, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Nyatwali.

Aliwataja wavuvi waliokufa kuwa ni mmiliki wa mtumbwi huo, Kulwa Rhobati (31), Muhoja Munze (32) na Sengelema Abdallah (31), ambao wote ni wakazi wa Mtaa wa Tamau, mjini Bunda.

Alisema miili ya watu hao ilipatikana kutokana na msaada mkubwa wa mafuta yaliyoletwa na mdau mmoja wa shirika lisilokuwa la kiserikali pamoja na Kampuni ya Mwanza Huduma.

Mkurugenzi wa shirika lisilokuwa la kiserikali la Zinduka, Maximillian Madoro, alisema baada ya kupata taarifa ya tukio hilo aliwasiliana na Mkurugenzi wa Kampuni ya Mwanza Huduma na kwenda katika eneo la tukio, na kutoa msaada wa chakula na mafuta ili kuweka kwenye mitumbwi ya injini kwa ajili ya kutafuta watu hao.

Madoro alisema kuwa utu ni muhimu na ndiyo maana wameguswa na tukio hilo na kuamua kutoa msaada huo.

Diwani wa kata hiyo, Ndovu Chacha, aliwashukuru wadau waliotoa msaada huo pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Bunda, Lydia Bupilipili, kwa kufika mapema katika eneo la tukio na kutoa pole.

***Imeandikwa na Julieth Mkireri, Bagamoyo na Ahmed Makongo, BUNDA***

# Takukuru kuchunguza misaada ya corona

**Na Enock Charles**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), imesema kuwa itafuatilia kwa karibu misaada yote inayotolewa kwa ajili ya kusaidia jitihada za kupambana na corona kuhakikisha hakuna vitendo vya rushwa.

Mkurugenzi Mkuu wa taasisi hiyo, Bregedia Jenerali John Mbungo, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari, ofisini kwake.

Alisema Takukuru inaomba ushirikiano wa wananchi kwa kutoa taarifa mbalimbali zenye viashiria vya rushwa katika maeneo yao katika utoaji wa misaada hiyo.

"Tungependa mtambue kwamba Takukuru iko macho katika kufuatilia matumizi ya misaada mbalimbali inayotolewa na wadau katika kipindi hiki cha janga la corona," alisema Mbungo.

**"Tungependa mtambue kwamba Takukuru iko macho katika kufuatilia matumizi ya misaada mbalimbali inayotolewa na wadau katika kipindi hiki cha janga la corona," alisema Mbungo.**

**YAOKOA BIL. 11 ZA WAKULIMA**

Alisema Takukuru imeokoa Sh. bilioni 11 kati ya 103 za vyama vya ushirika na kuzirejesha kwa wakulima, baada ya kufanya uchunguzi na kufungua kesi mahakamani kwa wale ambao hawakutoa ushirikiano wa kurejesha fedha hizo.

Kadhalika, alisema Sh. bilioni 92 bado zinachunguzwa na kuvitaka vyama sugu vinavyodaiwa fedha hizo za wakulima kurejesha haraka iwezekanavyo.

Mkurugenzi huyo aliitaja mikoa ambayo vyama vilirejesha fedha na kiasi kwenye mabano kuwa ni Njombe (Sh. 4,049,294,856), Lindi (Sh. 1,361,209,809), Ruvuma (Sh. 1,078,027,619), Kilimanjaro (Sh. 108,005,700), Manyara (Sh. 81,148,617), Kinondoni (Sh. 33,728,000), Katavi (Sh. 73,172,500) na Pwani (Sh. 347,514,550).

Mingine ni Mbeya (Sh. 107, 450,790), Iringa (Sh. 714,417,198), Singida (Sh. 43,194,500), Simiyu (Sh. 83,972,750), Ilala (Sh. 50,610,000), Arusha (Sh. 64, 435,350), Kigoma (Sh. 36,150,400) na Tanga (Sh. 10,842,480).

Mkurugenzi huyo alivitaja vyama vya ushirika sugu kwa kufuja fedha za wakulima kuwa ni Chama cha Kyeku kilichopo jijini Mbeya, kinachodaiwa Sh. milioni 476, Chama cha Korosho cha (Tanecu), kilichopo mjini Mtwara kinachodaiwa Sh. milioni 359, Neema Saccos, mkoani Njombe kinachodaiwa Sh. milioni 234.

Vingine ni Mamcu cha Mtwara, kinachodaiwa Sh. bilioni 2.5, Runali cha Nachingwea kinachodaiwa Sh. milioni 856 na Chama cha SSULT cha jijini Dar es Salaam kinachodaiwa zaidi ya Sh. bilioni 4.8.




**Bonite Bottlers Ltd** inayo furaha kuwaletea **Maji ya Kilimanjaro katika ujazo mkubwa wa LITA 6, LITA 12 na LITA 18.9.** Tumewekeza katika mitambo ya kisasa ya kuzalisha maji katika ujazo mkubwa ili kuwawezesha wateja, wanywaji na wadau wetu kupata maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani, maofisini na kwenye taasisi mbalimbali.

**UPATIKANAJI:-**

- Maji ya Kilimanjaro katika ujazo mkubwa yanapatikana kwenye depoti zetu zote zilizoko mikoani, maduka na wauzaji wa jumla nchi nzima.
- Kwa Wateja wetu wa Mkoa wa Dar es Salaam, unaweza kununua maji ya kunywa ya Kilimanjaro ukiwa nyumbani kwa njia ya mtandao kupitia makampuni ya usambazaji bidhaa tunayoshirikiana nayo ambayo ni Shoponline Tanzania **www.shoponline.co.tz** na Piki Deliveries **www.piki.co.tz** .

Ni matumaini yetu mtaendelea kutuunga mkono kwa kuburudika na maji kutoka kilele cha Afrika.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI:**

**Moshi:** +255 755851170 au +255 27 2754422/7, **Arusha:** +255 756339532 au +255 27 2544876, **Dar: +255 754635988 au +255 22 700450/655, Morogoro:** +255 782546090, **Dodoma:** +255 787495439, **Karatu:** +255 757673123, **Babati:** +255 765459199, **Singida:** +255 755271963, **Tanga:** +255 763407979, **Mbeya:** +255 757266235, **Mwanza:** +255 742099191, **Nzega:** +255 746031412

**MAJI YA KUNYWA YA KILIMANJARO NI MAJI YA KUAMINIKA KILA SIKU!**

# Mpango: Wizara kubaini athari ugonjwa corona

**Na Gwamaka Alipipi, DODOMA**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, amesema wizara yake inakamilisha uchambuzi wa taarifa mbalimbali za kisekta, ili kubaini kiwango cha athari za mlipuko wa ugonjwa wa virusi vya corona katika uchumi, kuainisha mikakati ya muda mfupi, kati, mrefu ya kukabiliana nazo.

Amesema katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, mwaka huu, kitengo cha udhibiti fedha haramu kilipokea na kuchambua taarifa za miamala shuku 724, kati ya hiyo, taarifa fiche 61 zimewasilishwa kwenye vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria kwa ajili ya uchunguzi.

Alitoa maelezo hayo jana bungeni mjini Dodoma, wakati akiwasilisha makadirio na matumizi ya wizara yake kwa mwaka wa fedha 2020/21, akiliomba Bunge kuidhinisha Sh. trilioni 12.39.

Alisema kitengo hicho kimeingia makubaliano na vitengo vya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Japan na Jamhuri ya Kongo kwa ajili ya utekelezaji wa mikakati ya kimataifa ya udhibiti wa utakasishaji wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi.

Dk. Mpango alisema: "Katika mwaka 2020/21, kitengo cha udhibiti fedha haramu kinatarajia kuboresha na kuhuisha mifumo ya upokeaji wa taarifa za miamala shuku na kusimamia utekelezaji wa mpango kazi wa matokeo ya tathmini ya kitaifa ya mifumo ya kudhibiti utakasishaji fedha haramu na ufadhili wa ugaidi."

Alisema kwa mwaka wa fedha 2019/20 sekta zilizoongoza katika ukuaji ni pamoja na uchimbaji wa madini na mawe asilimia 17.7, ujenzi asilimia 14.1, sanaa na burudani asilimia 11.2; na usafirishaji na uhifadhi wa mizigo asilimia 8.7.

Kuhusu deni la serikali, Waziri Mpango alisema, serikali inaendelea kusimamia deni la serikali kwa kuzingatia Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada sura 134.

Alisema kipaumbele ni kukopa kutoka kwenye vyanzo vyenye masharti nafuu na fedha zinazopatikana kuelekezwa kwenye miradi ya maendeleo, hususani inayochochea ukuaji wa shughuli za kiuchumi na maendeleo ya watu.

"Vile vile, wizara inaendelea kuhakikisha kuwa, madeni yote yanayoiva yanalipwa kwa wakati hadi kufikia Machi 2020, serikali ilifanikiwa kulipa deni lote lililoiva lenye thamani ya Sh. trilioni 6.19," alisema Dk. Mpango na kuongeza:

"Kati ya kiasi hicho, deni la ndani ni Sh. trilioni 4.06 ikijumuisha riba Sh. trilioni 1.08 na mtaji Sh. trilioni 2.98, vile vile, deni la nje ni Sh. trilioni 2.13 ikijumuisha riba ya Sh. bilioni 636.75 na mtaji Sh. trilioni 1.49," alisema Dk. Mpango.

Alisema kati ya Julai 2019 na Machi 2020, wizara imelipa mafao na pensheni kwa wastaafu wa serikali 57,605, mirathi kwa warithi 1,006 na malipo ya kiinua mgongo kwa watumishi 457 wa serikali walio kwenye mikataba.

Pia, katika mwaka 2020/21, Wizara ya Fedha na Mipango inaomba kuidhinishiwa Sh. trilioni 12.39 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo.

Alisema kati ya kiasi hicho Sh. trilioni 11.73 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. bilioni 659 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Alisema kati ya matumizi ya kawaida, Sh. trilioni 10.48 kwa ajili ya deni la serikali, Sh. bilioni 750.29 matumizi mengineyo na Sh. bilioni 510 kwa ajili ya mishahara na marekebisho ya mishahara.



Mchuuzi wa ndizi akimhudumia mteja wake katika Soko la Temeke, jijini Dar es Salaam jana. Mkungu mmoja wa ndizi uliuzwa kwa bei ya 9,000/- hadi 11,000/- kulingana na ukubwa wake. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mahakama Kuu yaruhusu dhamana kwa Nchambi

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Shinyanga, imesema kuwa Mbunge wa Kishapu (CCM), Suleiman Nchambi, ana haki ya kupewa dhamana kwa masharti katika kesi ya uhujumu uchumi.

Mbunge huyo anakabiliwa na makosa 12.

Akitoa uamuzi wa maombi ya dhamana hiyo jana, Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Shinyanga, Phocus Mkeha, aliyataja masharti ya dhamana kuwa ni kusaini bondi ya Sh. milioni 50 na mdhamini wake bondi ya Sh. milioni 10, pamoja na kushikilia hati yake ya kusafiria.

Vile vile, Jaji alisema maamuzi ya utoaji wa dhamana hiyo ameyarudisha katika Mahakama ya Wilaya ya Shinyanga mahali kesi yake ya msingi ilipoanzia, na kwamba ndiyo watasimamia masharti ya utoaji wa dhamana hiyo.

Mei 13, mwaka huu wakili wa mshtakiwa huyo, Frank Mwalongo, aliwasilisha hati ya maombi ya dhamana dhidi ya mteja wake katika Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Shinyanga, kutokana na Mahakama ya Wilaya kutokuwa na uwezo kisheria kusikiliza kesi za uhujumu uchumi wala kutoa dhamana ya kiasi kisichozidi Sh. milioni 10.

Mbunge huyo alifikishwa mahakamani Mei 8, mwaka huu, mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Ushindi Swalo, na kusomewa mashtaka 12 ya uhujumu uchumi, kwa kumiliki silaha (bunduki), na risasi kinyume na sheria.

Kesi hiyo ilipangwa kusikilizwa Mei 11, katika Mahakama hiyo ya wilaya, lakini iliahirishwa hadi Mei 25, mwaka huu, kutokana na kutokuwa na uwezo wa kusikiliza kesi za uhujumu uchumi.

## Gasco kutumia kamera kufuatilia miundombinu

**Na Romana Mallya**

KAIMU Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni tanzu ya gesi Tanzania (Gasco), Baltazar Mrosso, amesema wanatarajia kutumia kamera za juu (drone camera) kuyabaini maeneo ya miundombinu ya bomba la gesi asilia yaliyoathiriwa na mvua ili yaweze kufanyiwa matengenezo.

Gasco ni kampuni tanzu ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), ambayo inafanya uendeshaji, matengenezo ya miundombinu yote ya gesi asilia ya serikali.

Mrosso aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam baada ya kutembelea moja ya eneo la bomba hilo lililopo Kinzudi, Kata ya Goba jijini Dar es Salaam ambalo limeathiriwa na mvua na kusababisha udongo uliokuwa umelifunika kuzolewa na maji.

Alisema wanatarajia baada ya mvua kuisha watapita maeneo yote yaliyoathiriwa na maji ili kuyafanyia matengenezo.

"Mpaka sasa yapo maeneo kama sita ambayo tuna taarifa zake yamepata madhara na yote yatarekebishwa kwa utaratibu. Yale yaliyoathirika kidogo yatarekebishwa haraka na yale yaliyoathirika zaidi makandarasi watatumika kuyatengeneza ili mvua nyingine zikija yasipate madhara," alisema.

Aliyataja maeneo ambayo yameathiriwa ambayo mpaka sasa wanataarifa zake ni Dar es Salaam, Mkuranga na Mtwara.

Hata hivyo, aliwatoa wasiwasi wananchi wa eneo hilo waliolitembea kuwa athari zilizotokea hazina madhara kwao.

Mrosso aliwakumbusha wananchi kuwa hakuna anayeruhusiwa kufanya shughuli yoyote kwenye miundombinu hiyo na ikitokea wamefanya hivyo serikali za mtaa huwasiliana nao na hatua shahiki huchukuliwa.

"Wananchi waliopitiwa na miundombinu hii wanatakiwa kuwa walinzi na kutofanya shughuli zozote za kijamii kwenye miundombinu hii.

"Kuna mabomba yanayopitisha gesi yenye mkandamizo wa hali ya juu ambayo ni mabomba ya chuma na yale yanayopitisha gesi yenye mkandamizo wa chini yaliyotengenezwa kwa plastiki hayo yanatumika kusambaza gesi kwenye majumba ya watu na viwandani."

Alisema hivyo kama mwananchi atapika juu ya bomba hilo la plastiki maana yake moto ukienda chini unaweza kuleta madhara ndiyo maana haturuhusu watu kufanya shughuli na zipo alama kuonyesha mabomba yalikopita.

Mkuu wa Kitengo cha Ulinzi na Usalama Miundombinu ya gesi asilia Gasco, Rodrick Ntabuoyo, alisema bomba hilo limepita mikoa minne ambayo ni Mtwara, Lindi Pwani na Dar es Salaam.

Alisema katika miundombinu hiyo upo ulinzi unaozuia shughuli zozote kufanyika ikiwa ni pamoja na ufugaji, kilimo na ujenzi wa nyumba.

Naye, Mwenyekiti wa Serikali za Mitaa Kinzudi, Kata ya Goba, Edward Mbwiga, alisema wamekuwa wakishirikiana na Gasco na TPDC kwa kutoa taarifa kwao kama kuna uvunjifu wowote utaratibu ndani ya miundombinu hiyo ili iendelee kubaki salama.

# Mahakama Kuu yatupa kesi kupinga Katiba

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA Kuu, Kanda ya Dar es Salaam imetupilia mbali kesi ya kikatiba iliyofunguliwa na taasisi mbili zisizo za serikali dhidi ya kupinga marekebisho katika Sheria ya Kampuni Sura ya 212, Sheria ya Asasi zisizo za Serikali Sura ya 337 na Sheria ya Usajili wa Wadhamini Sura ya 318.

Marekebisho hayo yalikuwa yanahusu kuweka tafsiri mpya ya maneno kampuni na asasi katika sheria husika.

Kadhalika, kuzitaka asasi zote zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Kampuni ambazo hazikuwa na malengo ya kibiashara, kujisajili chini ya sheria na iwapo zingeshindwa kufanya hivyo ndani ya muda wa miezi miwili zingehesabika kuwa zimefutiwa usajili wake.

Katika kesi hiyo ya kikatiba iliyosajiliwa kwa namba 21/2019, ilifunguliwa Agosti 29, 2019 na Taasisi isiyo ya kiserikali ya Centre for Strategic Litigation, inayomilikiwa na Wakili wa Kujitegemea, Jebra Kambole pamoja na Asasi ya Change Tanzania Limited, inayomilikiwa na Maria Sarungi.

Uamuzi huo ulisomwa juzi na jopo la majaji watatu likiongozwa na Jaji Mfawidhi, Lameck Mlacha, akisaidiana na Yose Mlyambina na Stephen Magoiga.

Jaji Mlacha alisema walalamikaji katika maombi hayo wameshindwa kuwasilisha hoja za msingi kutetea maombi yao.

Alisema analitupilia mbali shauri hilo na kuelekeza taasisi hizo kulipa gharama za uendeshaji wa shauri hilo kwa serikali.

Katika hoja za serikali ilipinga maombi hayo kwa hoja mbalimbali ikiwamo walalamikaji kushindwa kubainisha na kuithibitishia mahakama athari ambazo zinatokana na marekebisho hayo ya sheria kwa kiwango kinachostahili katika mashauri ya kikatiba.

Ilidai maombi yaliyowasilishwa mahakamani yaliegemea zaidi katika hisia za walalamikaji na sio maslahi mapana ya umma.

Katika maombi yao, asasi hizo zilipinga marekebisho ya sheria husika kwa msingi kuwa yalikiuka ibara za 13(1), (2), (6) (a),(b); 20(1) na 29(1) na (2) za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kile kilichodaiwa kuwa marekebisho hayo yanakinzana na haki ya usawa mbele ya sheria, uhuru wa kujumuika na haki ya kufaidi haki za msingi za binadamu.



Baadhi ya wakazi wa kijiji cha Buira, Wilaya ya Musoma, mkoani Mara, wakikusanya mchanga juzi, kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu wa Shule ya Msingi Buira, ili kuwaondolea changamoto ya kuishi katika nyumba za kupanga. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Jela miaka 6 kwa kuomba rushwa 150,000/-

**Na Gurian Adolf, KATAVI**

MAHAKAMA ya Wilaya ya Mpanda, mkoani Katavi imemhukumu karani wa kituo cha kununulia pamba cha Amcos ya Mpanda Kati, Issa Bidah, jela miaka sita au kulipa faini ya Sh. 1,000,000 baada ya kumtia hatiani kwa kosa la kuomba na kupokea rushwa ya Sh. 150,000 kutoka kwa mkulima wa pamba.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Gosper Luoga, baada ya kuridhika na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka ulioongozwa na Mwanasheria wa kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Simon Bucha.

Mshtakiwa alipewa hukumu hiyo baada ya kupatikana na hatia ya kutenda kosa kinyume na kifungu cha sheria namba 15 (1) (a) na(2) sura ya 329 cha Sheria ya Takukuru namba 11 ya mwaka 2007 na marekebisho yake kufanyika mwaka 2018.

Awali, kwenye kesi hiyo, Mwanasheria wa Takukuru, Buchwa alidai kuwa mshtakiwa alitenda kosa hilo Desemba 12, mwaka jana huko kwenye kituo cha kuuzia pamba kilichopo Kijiji cha Kaseganyama, wilayani Tanganyika.

Alisema, Didah akiwa karani wa Amcos ya Mpanda Kati, alipewa jukumu la kuhakikisha pamba kwenye kituo cha Kaseganyama inanunuliwa na Amcos, hivyo alishawishi kuomba na kupokea rushwa ya Sh. 150,000 kutoka kwa mkulima wa pamba, Lois Moris, ili amruhusu kupima pamba yake na aiuze kwenye Amcos hiyo.

Siku ya tukio hilo mshtakiwa anadaiwa kuomba kupewa rushwa kiasi hicho cha fedha ili aweze kumsaidia mkulima huyo kumpa upendeleo wa kulipwa mapema malipo yake pindi yatakapo kuwa yametoka.

Buchwa aliiambia mahakama kuwa karani huyo alipokea rushwa kiasi hicho cha fedha kwa wakulima mbalimbali na hakuweza kuwapatia risti yoyote na wala kuwasainisha sehemu yoyote.

Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Luoga baada ya kusikiliza pande hizo mbili za mashtaka na upelelezi, aliiambia mahakama kuwa kutokana na ushahidi uliotolewa, mshtakiwa amepatikana na hatia hivyo kabla ya hukumu kutolewa nafasi ya kujitetea kama anasababu yoyote ya msingi ya kuomba apunguziwe adhabu na mahakama.

Katika utetezi wake mshtakiwa aliomba mahakama impunguzie adhabu kwa kuwa ana familia kubwa inayomtegemea na pia hali ya afya yake kutokuwa nzuri.

Baada ya utetezi huu Mwanasheria wa Takukuru Buchwa, aliiambia mahakama kuwa hana rekodi yoyote ya mshtakiwa kutenda kosa kama hilo hivyo aliiomba mahakama itoe adhabu kwa kuzingatia sheria.

Hakimu Luoga alisema mahakama inamhukumu kutumikia kifungo cha miaka mitatu jela kwa kila kosa hivyo kwa makosa hayo mawili anahukumiwa kwenda jela jumla ya miaka sita au kulipa faini kwa kila kosa Sh. 500,000.

# Wazazi wasisitizwa kulinda watoto, wazee

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, amewasisitiza wazazi na walezi kutumia kipindi cha mapambano dhidi ya ugonjwa wa Covid -19 kufuatilia na kuwalinda watoto wao pamoja na kutathmini fursa zilizopo katika kipindi hiki.

Pia amezitaka familia kufuatilia hali ya kiafya ya wazee ikiwamo kuzingatia na kufuatilia hali zao za lishe.

Ummy alitoa kauli hiyo jana ikiwa ni maadhimisho ya Siku ya Familia Duniani ambayo hufanyika Mei 15, kila mwaka.

Alitoa wito kwa jamii katika kipindi hiki kutowanyanyasa waliopata maambukizo ya corona.

"Niwaombe wazazi na walezi muwe karibu na familia zenu hasa watoto na wazee na punde mnapobaina dalili za ugonjwa wa corona kwao, toeni taarifa ili hatua stahiki zichukuliwe," alisema Ummy.

Aliwataka wazazi kubuni michezo mbalimbali itakayokuwa kivutio kwa watoto wao ya kuwasaidia kuendelea kujifunza wakiwa nyumbani badala ya kudhurura mitaani.

Alisema katika kipindi hiki ambacho shule zimefungwa ikiwa ni njia ya kuwaepusha na maambukizo ya virusi vya corona, ni vema watoto wakaandaliwa mazingira bora ya kufuatilia masomo kupitia vyombo vya habari na njia ya mtandao.

"Familia ni msingi wa ustawi wa jamii yoyote ile hivyo ni muhimu kuilinda ili kufikia maendeleo endelevu na kuhakikisha tunailinda na maambukizo ya virusi vya corona," alisema Ummy.

Kadhalika alisema, kutokana na umuhimu wa familia kwa ustawi wa jamii, wazazi na walezi wana kila sababu ya kubadilisha tabia, mitazamo na kuongeza maarifa, huku wakiongeza mbinu za kuiwezesha familia kukabiliana na changamoto mbalimbali zikiwamo za maambukizo ya virusi vya corona.

Alisisitiza umuhimu wa Watanzania kuendelea kufuata kanuni na maelekezo ya wataalamu wa afya ili kujikinga na kuwakinga wengine dhidi ya maambukizo ya ugonjwa wa Covid-19 husani kwa kujiepusha na mikusanyiko, kunawa mikono kwa kutumia sabuni na maji tiririka, kutumia vitakasa mikono, kuzingatia umbali wa mita moja kati ya mtu na mtu pamoja na kuvaa barakoa.

Alizitaka Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhakikisha zinaadhimisha siku hiyo kwa kutoa elimu kwa familia kuhusu namna ya kujikinga na maambukizo ya virusi hivyo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Idadi wachezaji wa kigeni nchini isitumiwe vibaya

BARAZA la Michezo la Taifa (BMT), limeanza kupokea maoni kutoka kwa wadau mbalimbali wa soka kuhusu idadi ya wachezaji wa kigeni wanaotakiwa kusajiliwa na timu za hapa nchini ndani ya msimu mmoja.

Kwa sasa kanuni zilizopitishwa na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kwa kuzingatia mapendekezo yaliyotolewa na klabu za Ligi Kuu Bara, zinataka timu moja kusajili wachezaji wa kigeni wasiozidi 10.

Lakini kanuni hiyo hiyo, ilielekeza klabu hizo kusajili wachezaji wageni ambao wanazitumikia nchi zao (Timu za Taifa), kwa malengo ya kuwapa changamoto ya kuwania namba kwenye kikosi cha kwanza.

Kipengele hiki kilizingatia kuifanya Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo ndio ina wachezaji wengi kutoka nje ya nchi kutokuwa 'jalala' la wachezaji walioachwa na timu nyingine na vile vile kuiongezea thamani.

Wachezaji wa kigeni wenye viwango vya juu, mbali na kulipatia Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kipato kupitia ada ya Dola za Marekani 2,000 (zaidi ya Sh. milioni nne), wanatakiwa wawe ni wenye uwezo wa kuzisaidia timu husika kufanya vizuri katika mashindano yote, timu yake iliyomsajili wanayoshiriki.

Lakini wachezaji wageni ambao watasajiliwa bila kufuata vigezo, huenda wakazigharimu klabu husika badala ya kuwapa kile walichokitarajia wakati wanawasajili.

Mbali na ushindani wa kuwania namba, pia usajili wao unalenga kuwapa 'kiu' wachezaji wazawa nao kujituma na kuongeza bidii ili kuwindwa na timu za mataifa mengine au kwa walioko katika madaraja ya chini kutakiwa na timu za ngazi ya juu.

Idadi hiyo iliongezeka kutoka wachezaji watano iliyokuwa awali, baada ya viongozi wa klabu za Ligi Kuu Tanzania Bara na Ligi Daraja la Kwanza kuridhia uamuzi huo.

Hata hivyo, bado katika kipengele hicho, klabu zimekuwa hazitekelezi vema usajili huo, kwa kuingia mikataba na wachezaji ambao hawachezi katika Timu za Mataifa wanayotoka kama ilivyopitishwa.

Tumeshuhudia klabu zikiwasajili wachezaji ambao hawajawahi kuchezea timu zozote za mataifa wanayotoka au wengine wakiwa wamekaa bila ya timu kwa muda mrefu, na matokeo yake kutumia Ligi Kuu Tanzania Bara kama sehemu ya kufanya mazoezi na kuinua upya viwango vyao.

Nipashe inazikumbusha klabu zenye uwezo na nia ya kusajili wachezaji wageni, kuhakikisha zinafanya mchakato huo kwa umakini wa kiwango cha juu.

Wachezaji wa kigeni ambao watakuwa na viwango bora kama ilivyo kwa Mzambia Clatous Chama anayeichezea Simba, Haruna Niyonzima kutoka Rwanda wa Yanga au Nicholas Wadada anayeitumikia Azam na Timu ya Taifa ya Uganda (Cranes), ndio aina ya nyota wanaotakiwa.

Haipendezi kuona klabu inasajili mchezaji wa kigeni, halafu yenyewe ikiwa haijiamini na ilichokifanya huku ikipa moyo kwa kumpa muda wa kuzoea ligi.


Kama ambavyo wachezaji wetu wa Tanzania wanafanya kwanza majaribio kabla ya kusajiliwa huko ughaibuni wanakokwenda kusaka timu, pia klabu za hapa nchini zisione vibaya kuwafanyia kwanza majaribio nyota wanaokuja na kuacha tabia ya kuwapa mikataba kabla ya kuwaona viwango vyao.

Utaratibu wa kuwafanyia majaribio uko duniani kote, kama mchezaji ana uwezo ataonekana kwenye majaribio, lakini kama 'sanaa' zitaendelea kuhusishwa kwenye usajili, safari ya mafanikio kwenye Ligi Kuu Bara itaendelea kukumbwa na changamoto ya kupokea wachezaji 'mizigo'.

Nipashe inawakumbusha viongozi wa klabu kutorudia makosa kwa kutoa mapendekezo yatakayoendana na mazingira na mahitaji halisi ya timu zao na vile vile kuweka mbele maslahi ya soka la Tanzania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Barnabas Maro

# Haki itumike Ligi Kuu

**HAKI** ni kitu au jambo ambalo mtu anastahiki kupata; utendaji, ufuataji na utumiaji wa kanuni katika kutimiza jambo; mali, milki. Kwa ufupi ni jambo linalomstahikia mtu; haki za binadamu.

Wakati serikali ikitafakuri kuhusu kuipa au kutoipa Simba ubingwa wa Ligi Kuu msimu huu, kumekuwa na mawazo mengi yanayotolewa na makundi mbalimbali.

Upande wa Simba, (kama ambavyo ungekuwa upande wa Yanga kama ingekuwa kwenye nafasi hiyo) unaomba timu yao itangazwe bingwa kwa kuwa ndiyo inayoongoza Ligi Kuu ikiwa na alama 71 baada ya kucheza mechi 28, kushinda 23, sare 2, kupoteza 3, ikifunga mabao 63 na kufungwa mabao 15.

Nadhani hali hii ndiyo iliyofanya m-bunge aliye mwanachama wa Simba apendekeze Ligi Kuu ifungwe na Simba wapewe kombe lao kwani ndiyo inayoongoza kati ya timu 20. Hoja hii aliitoa Bungeni! Ndivyo alivyotumwa na wapigakura wake?

Nasema hasha (sivyo kabisa)! Hata kama ingekuwa timu yangu (Yanga - timu ya wananchi) ndiyo inayoongoza, ningepinga wazo la kuipa ubingwa kabla ya kukamilisha michezo yote.

Naomba tukubaliane kutokubaliana kuwa 'kweli' ni uhakikisho wa jambo kama lilivyo; ingawa najua wapo watakaonibeza na kunifyonya. Hata hivyo wanapaswa kutambua kuwa msema kweli ni mpenzi wa Mungu.

"Kweli ikidhihiri, uongo hujitenga." Methali hii yatukumbusha kwamba ukweli wa jambo utokeapo, uongo unaolihusu hautambuliwi au hauna nafasi. Huweza kutumiwa kumnasihi mtu anayejaribu kusema uwongo waziwazi.

Mpaka Ligi Kuu ilipostmamishwa kutokana na woga wa maambukizi ya virusi vya corona, zilikuwa zimesalia mechi tofauti tofauti kati ya timu zinazoshiriki. Kwa ujumla, timu zote 20 za Ligi Kuu zatakiwa kucheza michezo 38 kila moja.

Kati ya timu 20 zinazoshiriki, 11 zimecheza mechi 29; timu nane zikiwamo Simba na Azam zikiwa zimecheza mara 28. Timu hizo zinafuatiwa na Yanga, timu pekee iliyocheza michezo 27.

Kwa nini nashauri Ligi Kuu iendelee? Ligi Kuu ya msimu ujao itakuwa na timu 16 tu. Katika msimamo huo, timu nne zitashushwa daraja, yaani hazitakuwapo kwenye Ligi Kuu msimu ujao.

Kwa maana hiyo timu zilizo mkiani, yaani Singida United, Mbao FC, Alliance FC na Mbeya City ndizo zilizo kwenye hatari ya kushushwa daraja kwa maana ya "Kwaheri Ligi Kuu."

Timu zilizo nafasi za juu ikiwamo Simba ambayo labda ifanyike miujiza ndio ishindwe kutwaa ubingwa kwa mara ya tatu mfululizo, ni Azam FC iliyo nafasi ya pili, Yanga kwenye nafasi ya tatu ikifuatiwa na Namungo ikiwa nafasi ya nne kutoka juu.

Ni wazi timu hizo tatu kila moja inaiombea nyingine mabaya ili ipate nafasi ya kwenda juu ili zishiriki michezo ya kimataifa.

Kama, kwa mfano, Simba ikiteleza na kushindwa kutwaa kombe lililo kwenye kizingiti cha jengo lao pale Msimbazi jijini Dar es Salaam, hapana shaka itakuwa katika nafasi ya pili. Hilo halina ubishi.

Ikiwa hivyo, kwa Simba itakuwa sawa na methali isemayo: "Ajabu ya shingo kukataa kulala kitandani." Ajabu inayorejelewa hapa, ni ya shingo kukataa kulala ingawa mwenyewe anataka kulala!

Hii ni methali ya kutumiwa kumrejelea mtu anayetaka kitu fulani lakini anajifanya hakitaki ilhali anakitaka!

Kama Simba wakishindwa kutwaa ubingwa (chondechonde, sio 'Ndoo' kama iandikwavyo magazetini), warudi na kujiuliza wamekosaje taji hilo msimu huu na hapo waweza kuuhusisha 'uchawi'.

"Amelaaniwa mtu yule amtegemeaye mwanadamu, amfanyae mwanadamu kuwa kinga yake, na moyoni mwake amemwacha Bwana. Maana atakuwa kama fukara nyikani, hataona yatakapotokea mema. Bali atakaa jangwani palipo ukame, katika nchi ya chumvi isiyokaliwa na watu." (Yeremia 17:5-6).

"Amebarikiwa mtu yule anayemtegemea Bwana, ambaye Bwana ni tumaini lake. Maana atakuwa kama mti uliopandwa kando ya maji, uenezao mizizi yake karibu na mto; hautaona hofu wakati wa hari ujapo, bali jani lake litakuwa bichi; wala hautahangaika mwaka wa uchache wa mvua, wala hautaacha kuzaa matunda." (Yeremia 17:7-8). Endapo Ligi Kuu itafutwa na Simba kupewa kombe, italeta manung'uniko kwa timu saba - tatu za juu zilizo chini ya Simba na nne za chini zitakazoshushwa daraja kwani msimu ujao watanakiwa kuwa na timu 16 tu. Itakuwa vilio na kusaga meno!

Ligi Kuu ichezwe hata bila watazamaji ili ikamilike. Tena iwe ndani na nje ili kila timu itumie fedha kwa usafiri wa kuzifuatia timu zingine na pia kufaidi viwanja vya nyumbani. Watazamaji waangalie kwenye runinga majumbani na 'vibanda hasara' mitaani.

*marobarnabas@yahoo.com*
*0784 334 096*

# Stakabadhi ghalani yawakomboa wakulima ufuta Tunduru

**Na Stevie Chindiye, TUNDURU**

JUMLA ya kilo 273,324 za ufuta zimeuzwa na wakulima wa Wilaya ya Tunduru, kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani katika mnada wa kwanza uliofanyika katika msimu wa mwaka 2019/2020.

Mnada huo ulifanyika katika viwanja vya ofisi za Chama cha Ushirika cha Mlingoti Magharibi (Amcos) na kuhusisha jumla ya wanunuzi watano, na watatu kati yao walishinda kununua ufuta huo kwa wastani wa bei ya Sh. 2,240 kwa kilo.

Katika mnada huo jumla ya Sh. 612,312,800 zilipatikana na kwamba zitasambazwa kwa wakulima waliokubali kuuza ufuta wao kupitia mfumo huo.

Kaimu Ofisa Ushirika wilayani Tunduru, George Bisani, alisema kuwa fedha hizo zinatarajiwa kuingizwa kwa wakulima waliokubali kuuza ufuta wao kupitia mfumo huo baada ya wanunuzi hao kuingiza fedha katika vyama vya ushirka vya wakulima vilivyokusanya zao hilo.

Awali, Meneja wa Chama Kikuu cha Ushirika wa Wakuliwa wilayani humo (TAMCU), Imani Kalembo, aliwataka wakulima walioshirki kwenye mnada huo kuwa makini kusikiliza bei zinazosomwa kutoka kwenye barua za wanunuzi ili wachague bei kubwa kuliko zote.

Naye, Mkuu wa Wilaya ya Tunduru, Julius Mtatiro, pamoja na pongezi kwa wanunuzi hao, aliwataka kuhakikisha wanafanya malipo kwa haraka ili kufanikisha malipo ya wakulima kwa wakati.

Vile vile, alisema wilaya hiyo imeanza vizuri msimu huo kwa kuuza mazao ya wakulima kwa bei nzuri ambayo itawawezesha kumudu gharama za uendeshaji na kupata faida.



Mafundi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), wakikata bomba la inchi 30, kwa ajili ya kubadili kipande kilichochakaa katika eneo la Kiluvya Gogoni, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# H'shauri Kaliua yatoa zaidi mil. 400/- elimu, afya

**Na Tiganya Vincent, TABORA**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kaliua, imetoa Sh. milioni 416.2 ili kuunga mkono juhudi za jamii katika shughuli za maendeleo ya sekta ya elimu na afya kwa mwaka huu wa fedha.

Fedha hizo zimetolewa baada ya kuona mwitikio mkubwa wa wananchi wa kuunga mkono mpango wa halmashauri wa elimu ya kujitegemea kuleta maendeleo.

Kauli hiyo imetolewa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Dk. John Pima, wakati akitoa mada kuhusu umuhimu wa elimu ya kujitegemea katika kuharakisha maendeleo, kwenye mafunzo ya siku mbili ya waajiriwa wapya.

Alisema kati ya fedha hizo halmashauri hiyo imenunua mabati bando 300 Sh. milioni 82.3, saruji mifuko 2,400 kwa Sh. milioni 36.6 na mbao 2,072 za Sh. milioni 7.2.

Mkurugenzi huyo Mtendaji aliongeza kuunga mkono elimu ya msingi walitoa Sh. milioni 15, sekondari Sh. milioni 45 na katika ujenzi wa miundombinu ya afya, Sh. milioni 230.

Dk. Pima alisema baada ya uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua kusisitiza umuhimu wa elimu ya kujitegemea kwa wananchi, kumekuwapo na mwitikio mkubwa kutoka katika jamii ambao umewafanya kushiriki katika ujenzi wa miundombinu ya elimu na afya.

Alisema katika kutambua umuhimu wa elimu ya kujitegemea ndani ya mwaka huu wa fedha, wazazi katika shule za msingi, wamefyatua matofali zaidi ya milioni 1.9 na kujenga vyumba vya madarasa 93, matundu ya vyoo 69 na nyumba za walimu 11.

Dk. Pima alisema wanafunzi wamelima mashamba ya mazao mbalimbali kama korosho ekari 118, mahindi ekari 143, alizeti ekari 16, viazi ekari 41, karanga ekari 80 na mpunga ekari 23.

Alisema kwa upande wa sekondari jamii imefyatua tofali zaidi ya 600,000 na kujenga vyumba vya madarasa 56, matundu ya vyoo 36, ya mazao ekari 121, ufugaji mbalimbali, ekari 15 za korosho; miti ya mbao ekari 71.8, matunda ekari tano na miti ya vivuli miche 2,467.

Dk. Pima alisema katika mwaka ujao wa fedha wanatarajia kuwa na miradi ya kilimo kwa ajili ya chakula, kilimo kwa ajili ya biashara, upandaji miti kila shule na miradi ya matofali kila shule.

Akifunga mafunzo hayo ya siku mbili, Mkuu wa Wilaya ya Kaliua, Abel Busalama, aliupongeza uongozi wa halmashauri hiyo kwa kuamua kutekeleza kwa vitendo dhana ya elimu ya kujitegemea.

Alisema matokeo yake yameonyesha kuwa kupitia elimu ya kujitegemea halmashauri zinaweza kuwa na miradi ambayo inawaingizia kipato na kuondokana na kutegemea ruzuku toka Serikali Kuu.

Busalama alisema kuwa halmashauri inaweza kujenga majengo kwa ajili ya viwanda na kupangisha wawekezaji na kupata kodi na kuondokana na kutegemea zaidi kodi ya mazao.

## Wazee wa kimila waomba mizimu kuepusha corona

**Na Neema Hussein, KATAVI**

WAZEE wa kimila mkoani Katavi wamefanya maombi ya kuuombea mkoa na Taifa kuepushwa na janga la ugonjwa wa corona.

Maombi hayo yamefanyika juzi katika mti wa mzimu unaojulikana kwa jina la Katabi, ambalo ndiyo jina lililozaa Mkoa wa Katavi.

Wananchi pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Juma Homera, walioshiriki maombi hayo, walisema baadhi ya vitu ambavyo waliwahi kuomba katika mti huo na vikafanikiwa ni mkoa kukumbwa na janga la njaa, mtu kuoa au kuolewa, kukosekana kwa mvua, na watu kupata watoto.

"Tumekuja kwenye matambiko ya asili mzimu wa Katabi tunakuomba ulitupe hili gonjwa mbali lifuate jua, linapokwenda na watemi wakina Sigulu, mtufungulie hili mtupe nuru haya magonjwa yatutoke, tunaliombea taifa zima utuondolee gonjwa la corona," walisema wazee hao.

Mwenyekiti wa mila na desturi, Mkoa wa Katavi, Michael Lusambo, alisema jina hilo la mzimu Katabi ndiyo asili ya jina lililokuwa likitumiwa na Mtemi Beda, hata katika kupata Mkoa wa Katavi, walipiga kura kama uendelee kuitwa kwa jina hilo.

Mkuu wa Mkoa, Homera alisema wao kama serikali hawana dini ila watu wao wana dini na hawaamini katika matambiko, lakini watu wao wanaamini hivyo na ndiyo sababu ya yeye kushuhudia wazee hao wakifanya matambiko kuliombea taifa liepushwe na ugonjwa wa corona.

Alisema mzimu huo wa Katabi ambao unapatikana katika mti uliopo Ziwa Katavi unatumiwa na makabila mbalimbali ya mkoa huo, hivyo anaamini kupitia mzimu huo, Mungu atasaidia kuondosha janga hilo.

**"Tumekuja kwenye matambiko ya asili mzimu wa Katabi tunakuomba ulitupe hili gonjwa mbali lifuate jua, linapokwenda na watemi wakina Sigulu, mtufungulie hili mtupe nuru haya magonjwa yatutoke, tunaliombea taifa zima utuondolee gonjwa la corona," walisema wazee hao.**

# Wafanyakazi 1,500 wadai kuzuiwa kuingia kiwandani Morogoro

**Na Waandishi Wetu, MOROGORO**

WAFANYAKAZI wapatao 1,500 wa kiwanda cha kutengeneza nguo cha Mazava Fabric & Production East Africa Ltd kilichopo Manispaa ya Morogoro, wamezuiliwa kuendelea na kazi baada ya kuzuiwa kuingia kiwandani hapo kutokana na mgogoro baina yao na uongozi wa kiwanda.

Kuzuka kwa mgogoro huo kumekuja siku mbili baada ya menejimeti ya kiwanda hicho kutangaza kusitisha kwa uzalishaji kwa kipindi cha miezi mitatu kuanzia Mei 24, mwaka huu, kutokana na kuenea kwa ugonjwa wa homa kali ya mapafu (Covid -19), ulioathiri masoko yake ya nguo inazozizalisha katika nchi za Ulaya na Marekani.

Wafanyakazi hao walizuiwa kuingia kiwandani jana kufuatia tangazo lililowekwa lango kuu na wao kuamua kwenda kukusanyika eneo la kituo cha mabasi Komoa umbali wa zaidi ya mita 300 kutoka kiwandani kusubiri hatima yao.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, baadhi ya wafanyakazi wakiwamo, Firida Josephat, Aidan Emmanuel na Zainabu Omary, walidai taarifa za kufungwa kwa kiwanda hicho walipewa lakini kilio chao ni namna ya kuzipata stahiki zao.

Emmanuel, alisema, uongozi wa kiwanda uliwafahamisha kuwa watalipwa nusu mshahara katika miezi mitatu ya likizo, lakini changamoto inayowakabili ni kiasi kidogo cha fedha wanacholipwa na endapo watalipwa nusu ya mshahara haitatosheleza kwa mahitaji yao.

Kwa mujibu wa wafanyakazi hao, awali walitangaziwa kupewa posho ya asilimia 50 ya mishahara na mmiliki wa kiwanda hicho, jambo ambalo wao hawakubaliani nalo na kudai ni kinyume na makubaliano ya mikataba yao ya kazi.

Kwa upande wake, Farida Josephat, alidai wapo wanaolipwa Sh. 150,000 kwa mwezi na wengine kiwango cha Sh. 120,000 kwa mwezi na kwamba kwa mshahara huo anapaswa kulipwa nusu yake (Sh. 60,000) kila mwezi.

Alisema kutokana na muda uliowekwa wa miezi mitatu iliyokuwa imetolewa na mmiliki wa kiwanda hicho na kwamba wao walihitaji walipewe mshahara wote kama mkataba wa makubaliano ulivyosema.

Alidai kuwa, sababu zilizotolewa na mmiliki wa kiwanda hicho ni kukosa oda ya kuzalisha nguo kutoka kwa wateja wao wakuu wa jezi zinazozalishwa kiwandani hapo kutoka nchi za nje hasa Marekani.

Walidai uamuzi huo wa mmiliki umepingwa na wafanyakazi wote kwa kuwa wanahitaji kulipwa mishahara yao kamili katika miezi hiyo mitatu maana hawajui soko la nguo za michezo litategemaa kwa muda gani.

Akizungumzia hilo, Meneja Uzalishaji wa Kiwanda cha Mazava, Nelson Mchukya, alisema suala la kufungwa kwa kiwanda hicho awali lilishirikisha wafanyakazi wote.

Mchukya, alisema baadaye wafanyakazi hao walikiuka makubalinao na wao wakitaka wasitishiwe mikataba ya kazi, na sasa jambo lao tayari lipo Chama cha Wafanyakazi wa Viwanda (TUICO) na wameshapeleka malalamiko katika Tume ya Usuluhishi ili kupata ufumbuzi.

Wafanyakazi hao hadi jana walikuwa bado wako nje ya kiwanda hicho wakiomba kuzungumza na Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Regina Chonjo ili kupata muafaka wao.

Kutokana na sakata hilo, ulinzi mkali wa polisi uliimarishwa nje ya eneo la kiwanda na sehemu walipokuwa wamekusanyika wafanyakazi hao.

***Imeandikwa na Idda Mushi na Ashton Balaigwa**



Askari wa Jeshi la Polisi, wakiwa wameimarisha ulinzi baada ya wafanyakazi wa kiwanda cha kutengeneza nguo za michezo cha Mazava Fabric & Production East Africa LTD kilichopo Manispaa ya Morogoro, kujikusanya umbali wa mita zaidi 200 kutoka kiwandani hapo jana, kutokana na kuzuiwa kuingiza ndani kufanya shughuli za uzalishaji na viongozi wao, wakidai kupewa likizo ya miezi mitatu bila malipo kutokana na kinachodaiwa kuwa ni ukosefu wa soko la nje ya nchi. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

# Bunge la Afrika Mashariki kuja kivingine

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

BUNGE la Afrika Mashariki limesema licha ya nchi zao na dunia kukabiliwa na janga la ugonjwa wa corona, linajiandaa kukutana mwezi ujao kwa ajili ya kujadili na kupitisha bajeti ya mwaka 2020/21 ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Vile vile, kutokana na janga la kuenea kwa virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa Covid-19, watajadili makadirio ya bajeti hiyo na kuipitisha kupitia njia ya mtandao ambayo tayari wameanza kuitumia katika kipindi cha tishio la ugonjwa huo.

Akizungumza jana kwa njia ya mtandao na waandishi wa habari, Spika wa Bunge la Jumuiya hiyo (EALA), Martin Ngoga, alisema hawana budi kuendelea na shughuli zao za bunge licha ya tishio la ugonjwa huo ili kuwezesha utekelezaji wa masuala mengine kuendelea.

"Ili kutekeleza kikao hicho cha bajeti nimeunda kamati maalum ambayo kwa sasa inafanya kazi kupanga mikakati ya jinsi ya kufanya kikao cha bajeti ya Bunge la Afrika Mashariki linalokuja, ili kila mbunge aweze kuhudhuria na kushiriki kikamilifu," alisema.

Pamoja na kuandaa kikao cha bajeti bado haijajulikana kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya kuendesha jumuiya hiyo, japo vyanzo vya EAC vilifafanua kuwa sehemu kubwa ya makadirio ya bajeti hiyo itapelekwa kushughulikia magonjwa ya milipuko ukiwamo ugonjwa wa Covid-19.

Ngoga alisema pia juzi wabunge wa EALA waliendesha kikao kwa njia ya mtandao kwa kila mbunge katika nchi sita wanachama kuelezea juhudi zilizochukuliwa kwenye nchi zao katika kupambana na ugonjwa huo.

Katika mazungumzo hayo, upande wa wabunge wa nchini Kenya, walisema wao nchi yao serikali imefunga sehemu za miji mikubwa tangu wapate kesi ya kwanza iliyothibitishwa Machi 13, mwaka huu.

Pia walisema wamepiga marufuku mikutano ya hadhara, kufunga shule na kusitisha safari za ndege.

Walisema mji wa Nairobi, Mombasa, Kilifi na Kwale, inatiliwa mkazo katika kuweka zuio la mikusanyiko kutokana na viwango vya juu zaidi vya maambukizo.

Nchi ya Uganda wao walisema serikali imefunga shughuli za umma za mikusanyiko na kuweka mkazo kwenye upimaji wa Covid-19.

Upande wa Tanzania waliwasilisha video zilizoonyesha wabunge wao wakielezea hatua zilizochukuliwa nchini ni pamoja na kufunga shule, kuhakikisha kila penye mkusanyiko pana kimiminika na vitakasa mikono ili wananchi wajikinge na maambukizo.

Pia, walieleza kuwa serikali kwa sasa inaendelea na utafiti wa dawa ya matibabu waliopewa msaada toka nchini Madagascar kwa ajili ya kupambana na ugonjwa huo.

Rwanda walisema wanakabiliana na ugonjwa huo kwa kutumia uzoefu waliopata wakati wa janga la ebola.

# Ewura yatoa tuzo Mamlaka Maji, Moshi, Iringa, Mwanza

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (Ewura), imetoa tuzo na vyeti kwa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira Moshi, Iringa na Mamlaka ya Maji Mwanza, baada ya kuibuka kinara katika utoaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira.

Akizungumza jana jijini Arusha, wakati wa utoaji tuzo hizo, Meneja wa Kanda ya Kaskazini, Mhandisi Lorivii Long'idu, alisema Mamlaka ya Maji Moshi imeshika nafasi ya kwanza, Iringa wa pili na nafasi ya tatu imeshikwa na Mwanza.

Alisema Ewura ilitoa taarifa kwa umma Aprili 16, mwaka huu, kuhusu utendaji wa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira nchini kwa mwaka 2018/19, ikihusisha mamlaka za maji za mikoa 26, miradi minane na mamlaka za wilaya na miji midogo 83.

Pia, alisema taarifa hiyo ilibainisha utoaji wa huduma umeimarika katika kiwango cha maji yaliyozalishwa, idadi ya watu wanaopata maji, ubora wa maji, wateja wa maji na wateja wa mtandao wa uondoaji majitaka, uwiano wa wafanyakazi na idadi ya wateja, makusanyo na ufanisi wa ukusanyaji maduhuli.

Mhandisi Lorivii alisema, taarifa hiyo pia ilibainisha changamoto zinazozikabili mamlaka za maji ikiwamo kiwango kikubwa cha upotevu wa maji, kiwango kidogo cha maji yanayozalishwa ikilinganishwa na mahitaji na utoaji huduma ya uondoshaji majitaka usiokidhi mahitaji.

Taarifa hiyo iliainisha mapendekezo ya namna ya kukabiliana na changamoto hizo na kuboresha huduma za majisafi na usafi wa mazingira zinazotolewa na mamlaka za maji nchini," alisema.

"Katika kuchukua tahadhari dhidi ya Covid-19 na ili kuepuka mikusanyiko ya watu wengi, iliamuliwa mamlaka zilizofanya vizuri zipokee tuzo na vyeti, kupitia ofisi za Kanda za Ewura nchini kote, tofauti na ilivyokuwa inafanyika miaka iliyopita kwa viongozi wa Mamlaka za Maji zote, kukutana kwenye mkutano wa pamoja wa mwaka," alisema.

Alitaja mamlaka za miradi ya kitaifa zilizofanya vizuri kuwa ni Mamlaka ya Maji KASHWASA (Kahama, Shinyanga Water Supply Authority) iliyoshika nafasi ya kwanza, MANAWASA (Masasi-Nachingwea Water Supply Authority), nafasi ya pili na CHALINZE (Chalinze Water Supply Authority (nafasi ya tatu).

Alisema Mamlaka za Miji ya Wilaya na Miji Midogo zilizofanya vizuri ni Makambako (nafasi ya kwanza), Mikumi (nafasi ya pili) na Biharamulo (nafasi ya tatu).

Pia, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (Moshi) imeibuka kinara katika utoaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira katika ripoti ya mwaka 2018/19 kwa upande wa mamlaka za maji za mikoa 26.

Alisema Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Moshi, imefanya vizuri zaidi katika kufikia malengo ya kiutendaji utoaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira miongoni mwa mamlaka 26 za mikoa.

HABARI DODOMA

# DC ashauri uandikishaji Bima ya Afya Chemba

**Na Paul Mabeja, CHEMBA**

MKUU wa Wilaya ya Chemba mkoani Dodoma, Simon Odunga, ameushauri mfuko wa Bima ya Afya ya Jamii (CHF), kuandikisha wananchi kwa kutumia watoa huduma ngazi ya jamii badala ya maofisa mifugo na kilimo.

Odunga, aliyasema hayo wakati akipokea vifaa mbalimbali vilivyotolewa na Taasisi ya Mkapa ikishirikiana na serikali kwa ajili ya watoa huduma wa afya ngazi ya jamii katika vijiji 79 wilayani Chemba, ili kuwafikia wananchi kwa urahisi.

Alisema kipindi cha nyumba wakati wa uandikishaji wa wananchi kujiunga na CHF, iliyoboreshwa walitumika watu ambao hawana taaluma na kazi hiyo kutokana na kukosekana watu wenye sifa ya kutosha.

"Kuna kipindi tulikuwa na changamoto ya kuandikisha watu, hivyo ilibidi maofisa ugani, kilimo, watendaji wa kata wao ndio watumike kufanya kazi ya kuwaandikisha watu, hii ilisababisha kuwapo malalamiko mbalimbali," alisema Odunga.

Pia, alisema kwa kuwa wamepata watoa huduma ya afya ngazi ya jamii anashauri wao ndio watumike katika kazi hiyo kwa kuwa ni wanataaluma wa afya, watafanya kazi hiyo kwa ufanisi.

Akizungumzia kuhusu vifaa hivyo, Odunga alisema vitawasaidia watoa huduma hao kuwafikia wananchi kwa urahisi zaidi tofauti na ilivyokuwa awali bila kujali ni kipindi cha kiangazi, masika au usiku.

"Jamii ina shida kwenye masuala ya lishe, kwa kuwa wanalima mazao, lakini lishe inakuwa changamoto, na kuhusu huduma ya afya wengine wanatumia miti shamba na huduma za vituo vya afya ni lazima wapate, wakuwahamasisha ni hawa watoa huduma ya afya ngazi ya jamii," alisema.

Kwa upande wake Meneja Miradi wa Taasisi ya Mkapa, Gaddy Chuwa, alisema vifaa walivyokabidhi kwa ajili ya watoa huduma ni baiskeli 79, mabegi, tochi, myamvuli pamoja na vifaa vingine, vyote vikiwa na thamani ya zaidi ya Sh. 25 milioni.

Alisema katika wilaya hiyo awamu ya kwanza waliwaajiri watoa huduma wa afya 35, pamoja na vifaa na kila mmoja alipangwa kufanya kazi katika kijiji kimoja.

Alisema awamu ya pili wameajiri 79, ili kuvifanya vijiji vyote vya wilaya hiyo kuwa na watoa elimu ya afya ngazi ya jamii.

Vilevile alisema lengo la kufanya hivyo ni kila mtu apate elimu juu ya masuala ya afya kabla hajafika katika vituo vya kutolea huduma.

Mmoja wa wamtoa huduma ya afya ngazi ya jamii Martha Matonya, alisema vifaa walivyokabidhiwa vitawarahisisha kuwafikia wananchi kwa lengo la kuwapatia elimu na kusaidia kutimiza malengo ya taasisi hiyo pamoja na serikali yafikiwe.



Mbunge wa Viti Maalumu (CCM), Mariamu Ditopile, akizungumza na wajane wa Kata ya Chang'ombe, jijini Dodoma mapema wiki hii, baada ya kutoa msaada wa vyakula kwa ajili ya mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Kulia ni Sheikh wa Baraza Kuu la Waislam Tanzania (Bakwata), mkoa wa Dodoma, Mustaph Rajabu. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Takukuru yakamata fedha zilizochukuliwa kinyume

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), mkoani Dodoma, imefanikiwa kuzikamata fedha za ujenzi wa ofisi ya Kata ya Mnadani, ambazo zilichukuliwa kinyume na utaratibu.

Fedha hizo zilipatikana baada ya Takukuru kuombwa kuingilia kati suala hilo, kutokana na ofisi hiyo kusuasua katika ujenzi wake.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alisema wamezirudisha fedha hizo ili kamati ya ujenzi iendelee na ujenzi huo.

Kibwengo, alisema kiasi cha Sh. milioni tano ambazo ziliibiwa na wajenzi na kusababisha kusimama kwa mradi huo.

Hata hivyo, alisema baada ya kuzibaini fedha hizo wameamua kuwarudishia ili zikaendelee na ujenzi wa ofisi hiyo ya kata.

Aliiagiza kamati hiyo kuhakikisha wanasimamia ujenzi huo na ofisi hiyo kukamilika kwa wakati.

"Nawaomba wananchi mwendelee kutoa taarifa pale mnapoona kuna viashiria vya rushwa lengo ni kusaidiana kutokomeza rushwa," alisema Kibwengo.

Naye Diwani wa Kata ya Mnadani, Farida Mbarouk, alisema anaishukuru Takukuru kwa kuwasaidia kupata fedha hizo ambazo zitaendeleza ujenzi wa ofisi hiyo.

Mbarouk, alisema fedha hizo zimekwamisha ujenzi huo ambao ungekuwa umeisha na wafanyakazi wamehamia.

Alisema wamejipanga kuhakikisha wanakamilisha ujenzi huo ili ofisi hiyo ianze kutumika kwa ajili ya kuwahudumia watu.

Pia, alisema bila taasisi hiyo wasingezipata fedha hizo ambazo ziliibiwa na watu waliokuwa wakijenga ofisi hizo ambazo ni msaada mkubwa kwa wakazi wa eneo hilo.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi, Matwiga Kyatya, alisema wanashukuru kupata fedha hizo ambazo wanaamini zitakamilisha ujenzi huo.

Alisema yeye kama Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi anaamini atasimamia vizuri na jengo hilo litasimama ili kutumika kwa wakazi wa eneo hilo.

# Jafo azindua kituo cha afya Sunya

**Na Augusta Njoji, KITETO**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amezindua kituo cha afya cha Sunya kilichopo wilayani Kiteto, mkoani Manyara na kuwataka wataalamu wa afya kujipanga katika kutoa huduma nzuri.

Aliwataka wananchi kuhakikisha wanalinda miundombinu ya kituo hicho ili dhamira ya serikali iliyopo ya kusogeza huduma za afya karibu na wananchi iweze kutimia.

Akizindua kituo hicho jana wilayani humo, Jafo alisema wilaya hiyo ilikuwa na changamoto nyingi ikiwamo kukosekana kwa kituo cha afya katika Kata ya Sunya, hali iliyowalazimu wakazi hao kusafiri umbali mrefu.

"Changamoto mojawapo ilikuwa ni ukosefu wa kituo cha afya na hivyo kulazimu wananchi kwenda wilayani Kilindi mkoani Tanga au kusafiri kilomita 125 kufuata huduma katika hospitali ya wilaya," alisema Jafo.

Alisema kituo hicho ni miongoni mwa vituo vilivyopewa kiasi cha Sh. milioni 400 na ujenzi umekamilika kwa kiwango alichoridhika nacho.

"Niwaombe wananchi mshirikiane katika kutunza miundombinu ya kituo hiki, sitarajii nikija hapa nikute mmeharibu koki hapana, kila mtu awe mlinzi wa mwenzake ili kituo hiki kiwe na manufaa kwa sisi na vizazi vyetu vijavyo," alisisitiza Jafo.

Alikagua pia ujenzi wa jengo la halmashauri na kumtaka mkandarasi Pacha Construction Ltd., kukamilisha ujenzi kwa wakati uliokusudiwa.

"Mkurugenzi ninachosisitiza hapa kazi ikamilike kwa wakati na niwaambie hili jengo likikamilika litakuwa ni miongoni mwa halmashauri zenye ofisi nzuri nchini, lakini wakati mwingine jitahidi gharama ziwe ndogo tofauti na hizi za sasa hivi," aliongeza Jafo.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya hiyo, Tumaini Magese, aliiomba serikali kuwaongezea vituo vya afya viwili ili kurahisisha upatikanaji wa huduma kutokana na ukubwa wa wilaya hiyo.

Alitaja changamoto iliyopo kwa sasa katika kituo hicho kuwa ni ukosefu wa umeme na hivyo kulazimika kutumia jenereta.

"Wilaya hii ni kubwa ina tarafa saba na imetawanyika sana, niiombe serikali itakapopatikana fursa basi tupate vituo vingine viwili ili visaidie wananchi wetu, suala la umeme bado ni changamoto, waziri wa nishati alikuja ameridhia kuleta umeme hivyo tunasubiria," alisema mkuu huyo wa wilaya.

Akitoa taarifa ya ujenzi huo, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kiteto, Tamimu Kambona, alisema ujenzi huo ulianza Januari 2018 na umekamilika mwaka 2019 kwa gharama ya zaidi ya Sh. milioni 510 na wananchi 38,273 wanatarajiwa kupata huduma katika kituo hicho.

# Wanaojipitisha majimboni wawakera wawakilishi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wamekerwa na tabia ya baadhi ya watu kujipitisha katika majimbo ya uchaguzi na kufanya kampeni kabla ya muda huku wakitaka wadhibitiwe.

Mwakilishi wa Jimbo la Kijitoupele, Ali Suleiman, aliyasema hayo jana na kueleza kuwa wapo baadhi ya watu wameanza kufanya kampeni katika majimbo ya uchaguzi kinyume na taratibu za CCM, huku wakitumia mwanya wa kutoa misaada kwa wananchi katika kipindi cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Aliiomba Mamlaka ya Kupambana na Kuzuia Rushwa Zanzibar (Zaeca), kueleza nguvu zake katika majimbo ya uchaguzi kwa ajili ya kuchunguza watu wanaojipenyeza huku wengine wakifanya kampeni za kutaka wachaguliwe.

"Mheshimiwa Naibu Spika wapo watu wameanza kuingia katika majimbo ya uchaguzi na kufanya kampeni kabla ya muda uliowekwa na chama, huku wengine wakijinadi...tunakiomba chama na Zaeca kudhibiti uvamizi huo," alisema.

Naye, Mwakilishi wa Jimbo la Makunduchi, Haroun Ali Suleiman, alitangaza nia yake ya kuwania jimbo hilo kwa kipindi kingine na kwamba atakuwa mwaka wake wa 25.

Alisema haipendezi kuona baadhi ya watu kujipenyeza katika majimbo ya uchaguzi kwa visingizio vya kutoa misaada kumbe huku wakifanya kampeni za chini kwa chini.

Alisema CCM imetoa mwongozo na kuwataka viongozi wa majimbo ya uchaguzi kuendelea na kazi ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi kwani muda wa kufanya kampeni haujafika.

Alisema tayari taasisi zilizopewa na majukumu ya kupambana na rushwa, zimeanza kulifanyia kazi suala hilo kikamilifu ikiwamo kuzunguka katika majimbo ya uchaguzi Unguja na Pemba.

"Mimi nakiomba chama kuwamulika watu wa aina hiyo kwa sababu wanakwenda kinyume na utaratibu wa maelekezo yake kusababisha vurugu, lakini mamlaka ya kupambana na rushwa tayari wameanza kazi ya kuwasaka watu wanaojipitisha kwa lengo la kutoa rushwa," alisisitiza.

Hivi karibuni, Zaeca ilieleza kuwa inafuatilia kwa karibu rushwa zozote kwenye majimbo mbalimbali na hatua kali zitachukuliwa.



Katibu wa CCM Mkoa wa Mwanza, Salum Kali, akipokea vifaa vya kujikinga na Covid- 19 kutoka kwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya chama hicho, mkoani humo, Flora Magabe, kwa ajili ya kuvisambaza katika ofisi saba za wilaya za CCM mkoani hapa, jana. **PICHA: ROSE JACOB**

## Kisiwa cha Pemba chahitaji Jaji

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi kutoka katika kisiwa cha Pemba wameiomba Wizara ya Katiba na Sheria, kupeleka jaji kisiwani humo, ili aweze kusikiliza kesi zinazofikishwa Mahakama Kuu kwa wakati.

Akichangia mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi kwa Wizara ya Katiba na Sheria, Mwakilishi wa Jimbo la Ole, Mussa Ali Mussa, alisema kisiwa hicho kina mikoa miwili na hivyo mahitaji ya kuwa na jaji ni makubwa.

Alisema uwapo wa jaji utawezesha kusikiliza kesi zenye uwezo wa kusikilizwa katika chombo hicho ikiwamo za mauaji.

"Kilio hiki ni cha muda mrefu matokeo yake ni kuwapo kwa mrundikano wa kesi ikiwamo zinazohusu matukio ya mauaji," alisema.

Mwakilishi wa Jimbo la Ziwani, Pemba, Suleiman Ali Makame, alisema kuwapo kwa jaji katika kisiwa cha Pemba kwa kiasi kikubwa kutasaidia wananchi kupata haki zao na hivyo kuimarisha utawala bora na haki za binadamu.

Alisema wapo watuhumiwa wanakata rufani, lakini wanachukua muda mrefu rufani zao kusikilizwa kutokana na kukosekana kwa jaji katika kisiwa hicho.

"Yapo malalamiko ya watuhumiwa kuchelewa kusikilizwa rufani zao mahakamani kwa sababu ya kukosekana kwa jaji ambaye hufika Pemba baada ya miezi sita kusikiliza rufani, tunahitaji kuwa na jaji anayeishi na kufanyakazi eneo hilo," alisisitiza.

# Zanzibar yaimarisha mahakama zake

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Zanzibar imesema inakusudia kuimarisha majengo ya mahakama kuwa ya kisasa na kutoa huduma zote muhimu ikiwamo msaada wa kisheria.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Katiba na Sheria, Khamis Juma Mwalimu, wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka huu wa fedha katika Baraza la Wawakilishi, visiwani humo.

Alisema ukarabati wa majengo ya Mahakama Kuu ya Vuga pamoja na Chake Chake, Pemba imeanza katika kuhakikisha kunakuwa na majengo bora yanayokidhi mahitaji.

Kwa mujibu wa waziri huyo, majengo hayo yakikamilika yatakuwa na uwezo wa kupokea idadi kubwa ya wananchi wanaofika kusikiliza mashauri mbalimbali.

Alisema kazi kama hiyo imefanyika katika mahakama za wilaya zilizopo Mkoa wa Kaskazini Unguja, Mfenesini pamoja na Makunduchi, Mkoa wa Kusini Unguja.

Kadhalika, alisema ujenzi wa jengo la kisasa la Mahakama Kuu huko Tunguu, Wilaya ya Kati Unguja, ujenzi wake unaendelea ambao unatarajiwa kukamilika mwakani baada ya jiwe la msingi kuwekwa na Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein. Kwa mujibu wa Mwalimu, serikali imeanza kutoa huduma za msaada wa kisheria kwa wananchi ikiwamo wasio na uwezo.

Vile vile, alisema mfumo wa msaada wa kisheria pamoja na wasaidizi wake umesaidia kwa kiasi kikubwa wananchi kupata ufumbuzi wa madai yao yaliyopo mahakamani.

Alisema Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), inaendelea na kasi ya upelelezi kwanza na utaratibu maalumu wa uendeshaji wa kesi za udhalilishaji wa kijinsia pamoja na zile za dawa za kulevya.

Mwalimu alisema utaratibu huo kwa kiasi kikubwa umepunguza mrundikano wa kesi mahakamani na kusikilizwa na imerudisha imani kwa wananchi katika vyombo vya sheria.

Alieleza kuwa kati ya mwaka 2019-2020 jumla ya kesi 19,382 zilifunguliwa katika mahakama mbalimbali visiwani humo, huku kesi 15,097 zikitolewa hukumu.

Alisema serikali imefanikiwa kuimarisha mhimili wa mahakama kwa kuongeza idadi ya majaji kutoka wanne hadi tisa, huku wakiwamo wanawake watatu.

Waziri huyo aliliomba baraza hilo kuidhinisha jumla ya Sh. 23,204,200,000,00 kwa kazi za kawaida na maendeleo kwa mwaka wa fedha 2020-2011.

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
UDANI
TELE



KATY PERRY, POLE YAKO, CORONA BADO IPO Ukurasa 14





## BIFU LIMEISHA

# Callisah, Ben Breaker kicheko

BIFU la wanamitindo maarufu nchini, Callisah na Ben Breaker, limefikia tamati baada ya serikali kuingilia kati na kutoa ushauri mzito.

Wanamitindo hao wamekuwa katika bifu kali kwa muda mrefu kwa kila mmoja akijigamba kuwa yeye ni zaidi katika fani hiyo.

Katika kipindi cha Friday Night Live, kinachorushwa na East Africa TV, Mei 8, mwaka huu, wawili hao walitoleana maneno makali kiasi kwamba Naibu Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Machezo Juliana Shonza, kutoa maoni yake yaliyosababisha bifu hilo kumalizika.

Waziri Shonza, aliwashauri vijana kuheshimiana na kuungana mkono kwa kila wanachokifanya kwa sababu mafanikio yao ni ya nchi kwa ujumla.

Callisah ambaye alionekana kukerwa kushirikishwa kwa Ben katika kipindi hicho, aliamua kuandika ujumbe wa kuomba radhi kwenye ukurasa wa mtandao wa Instagram, akisema ilikuwa ni jazba na hakudhamiria jambo hilo.

"Najua wengi mmekwazika kwa majibu yangu mabaya na kupaniki katika kipindi cha FNL ya #EATV kilichorushwa juzi, nichukue fursa hii kuomba radhi kwa wale wote waliokwazika sikuwa nategemea, baada ya kutafakari kwa makini nikagundua kweli nilikosea," ameandika.

Akaongeza "Pili nichukue fursa hii kumpongeza kijana mwenzangu Ben Breaker kwa juhudi kubwa anayofanya kwenye tasnia yetu na sisi wenyewe ndio wakushikana mikono. Mwisho nashukuru mama yetu mlezi Juliana Shonza, kwa ushauri wako mzuri juu ya sisi vijana, naahidi kutorudia tena na tutakua kitu kimoja, sanaa ni kazi na tuimarishe upend," ameongeza.

Baadhi ya mashabiki wake walimpongeza kwa hatua hiyo, wakisema kujitafakari na kutambua kosa ni kuonyesha jinsi gani alivyokomaa kisanii.

BASI SAWA

## Meja Kunta ajutia matendo yake

MAMBO yanamwendea kombo! Ndivyo anavyolalama mwanamuziki wa Singeli Meja Kunta, ambaye anasema kiki alizozifanya zimemsababishia mama yake mzazi kuathirika kiafya.

Akizungumza na eNewz, Meja Kunta amesema kwa sasa anafikilia njia sahihi ya kujitangaza na sio kujizulia mambo mabaya yanayosababisha hata mama yake kuwa mnyonge.



"Kwa upande wangu sizipendi, kitu ambacho ningeweza kufanya labda ni kuitisha watu au vyombo vya habari na nikaliongelea lile suala ili kujitoa na jinsi gani ya kujisafisha ili nisionekane mbaya".

Akaongeza "Kilichofanyika kimemuumiza sana na kimemsababishia matatizo hadi kwa mama yangu mzazi kwani hadi leo hii hayupo sawa amekuwa ni mtu wa kuanguka kiufupi hayupo sawa, kitu ambacho kinanipa mawazo sana kwa sababu sikuwahi kufirikia hata siku moja kama naweza kusababisha matatizo."

## P Mawenge kumchapa mwenzio sio dili

KUFUATI kuimarika kwa bifu kati ya marapa wakali P Mawenge na Nikki Mbishi, sasa mgogoro wao umevuka mipaka kiasi ambacho sasa wanataka kuingia ulingoni kuchapana.

Wasanii hao wa HipHop wameibua mjadala mkali kwenye mitandao ya kijamii, kutokana na kila mmoja kutoa ngoma inayomuimba mwenzake na kuvuta hisia mseto kwa mashabiki wao.



P Mawenge amesema yupo tayari kupambana ulingoni na Nikki Mbishi, ili kumtia adabu na kumwonyesha yeye ni zaidi.

"Nipo tayari na nipo vizuri, nafikiri watu wameshaanza kusogea juu ya jambo hilo na kuna harufu fulani nimeanza kuisikia, ikikubalika itakuwa vizuri zaidi kwa sababu, mwisho wa siku tunafanya hivi ili kutafuta maslahi zaidi, nipo tayari na nanyoosha mtu tukienda raundi tano zitatosha". Amesema P Mawenge.



## Mobetto ana watoto wawili bado bomba

MWANAMITINDO na mwanamuziki wa Bongofleva, Hamisa Mobetto, licha ya kuwa na watoto wawili wanaotokana na baba tofauti, watu hawakumchukulia vibaya na badala yake wanamuunga mkono kwa kila anachokifanya.

Hamissa ambaye ni balozi wa Afya ya Uzazi ya Sitetereki, wapo baadhi ya wasichana wanadhani kuzaa ni jambo rahisi, yeye anaweza kuwaambia kuwa ni suala gumu na linaweza kumtoa mtu njia sahihi.

"Nimepata bahati ya kutizamwa, kufuatiliwa na kuwa na mashabiki wengi, watoto wengi wa kike wananiangalia mimi na kudhani kwamba ni rahisi kuzaa mtoto, mwili umerudi na maisha yanaendelea na kuona mambo ambayo tunawaonyesha, lakini ni vigumu sana kuliko wanavyofikiria," ameeleza Hamisa Mobetto.

## Olita; Mapenzi hayapimwi kwa mzani

**Na Adam Fungamwango**

MAPENZI yana nguvu hapa duniani kuliko kitu kingine chochote. Mema na mabaya mengi hutokana na mapenzi tu. Filamu ya 'Olita' ni moja kati ya filamu za mapenzi yanayoonyesha nguvu hiyo.

Mama mmoja aliyekosa mtoto anaamua kwenda kwa waganga wa kijiji wamfanyie tambiko ili apate mtoto. Lakini sharti ni kwamba ni lazima mama yoyote kijijini hapo amtoke kafara mtoto wake ili mama hiyo apate mtoto.

Anajitokeza dada mmoja anamtoa mtoto wake mchanga sadaka ili mama huyo apate mtoto. Wakati hata mtoto hajatolewa kafara, mama alipata ujauzito.

Dada aliyetaka kumtoa kafara mtoto wake alikimbia kijijini hapo na mtoto wake. Mama anajifungua mtoto na kumwita Omaga.

Akiwa kijana anakuja kuchukuliwa na waganga wa kijiji kwa sababu hawajapata kafara yoyote. Lengo ni kutaka kumuua. Akiwa porini, Omaga anakimbia na kwenda kwenye kijiji cha mbali. Huko anaokotwa na msichana aitwaye Olita.

Kijana mwingine itwaye Moringe mwenye undugu wa karibu na Omaga, naye anaondoka kijijini hapo kwenda kumtafuta ndugu yake Omaga, naye anaangukia mikononi mwa pacha wa Olita, aitwaye Lorita.

Siku si nyingi, Omaga anaondoka nyumbani kwa kina Olita bila taarifa. Hii inamuumiza binti huyo kwa sababu tayari alishaanza kumpenda.

Olita anakwenda nyumbani kwa pacha mwenzake na kumkuta kijana anayefanana sana na Omaga.

Anachodhania ni kwamba ndugu yake amemnyang'anya mwanaume, hivyo ugomvi mkubwa unazuka.

Olita anachukua gongo na kumpiga kijana yule hadi kuzimia. Vita kali inawaka baina ya pacha hao, Olita na Lorita.

Hata hivyo kijana huyo alipozinduka, ukweli unabainika kuwa si Omaga, bali jina lake kamili ni Moringe.

Inabainika kuwa ni kweli wanafanana kwa sababu wana unasaba wa mtu na mdogo wake, lakini kwa mama tofauti.

Inagundulika kuwa Omaga ni kijana aliyezaliwa kwa dawa, lakini kuna masharti yalikiukwa, hivyo bado yuko kwenye hatari ya kufa.

Olita na mpenzi wake Omaga, Lorita na Moringe, wanaungana na kwenda kijijini kwao kukomesha tamaduni zilizopitwa na wakati. Mwishoni ndugu hao wa kiume, wanawaona pacha wa kike.







## Mmmh! Marioo kumbe huwezi

MWANAMUZIKI mkali wa Bongo Fleva, Marioo, yupo njia panda kukabiliana na maoni ya mashabiki wake ambao wanataka msanii huyo ajiunge kati ya lebo mbili, ambazo ni Kings Music Records ya Alikiba au Konde Gang ya Harmonize.

Wakati Kings Music Records, imeondokewa na wasanii wawili Cheed na Killy, upande mwingine Konde Gang imeanza vizuri na msanii wake mpya Ibraah Tz.

"Wakiniongelea mimi kuhusu kwenda sehemu hizo sio kitu kibaya sana, lakini binafsi sina mpango wa kusainiwa na lebo yoyote kwa sasa hivi, sana hapa Bongo". Amesema Marioo.

## Hawa ndio wanamuziki walioaga dunia wiki hii



MAFUMU BILAL

**Na Adam Fungamwango**

ILIKUWA ni wiki ya majonzi kwa tasnia ya muziki wa dansi nchini, baada ya kuondokewa na wanamuziki maarufu wanne ndani ya wiki moja tu.

Ni vifo vilivyoacha majonzi makubwa kwa mashabiki na wapenzi wa muziki ambao bado wako kwenye njia panda kuurudisha muziki wa dansi katika nafasi yake.

Wafuatao ni wanamuziki maarufu nchini ambao wamefariki kipindi cha ndani ya wiki moja tu.

**MAFUMU BILAL 'BOMBENGA'**

Ni mwanamuziki mkongwe na maarufu kabisa nchini. Huyu anajulikana zaidi kwa wimbo wa 'Maya' ambao aliuimba akiwa na bendi yake ya African Beat, ambao aliuchukua na kuutafasiri kutoka wimbo kama huo, 'Maya' ambao ulipigwa na TP OK Jazz ya Franco Luanzo Makiadi.

Mafumu alifariki Jumatatu jijini Dar es Salaam, baada ya kuugua ugonjwa wa kisukari kwa muda mrefu ambao ulisababishwa kukatwa mguu.

Mwanamuziki huyo ambaye ni mpuliza chombo cha saxophone, alipiga katika bendi mbalimbali kama Western Jazz, Dar International ya Marijani Rajab, Vijana Jazz, Maquiz Original, Tancut Almasi, Bima Lee, MK Group, kabla ya kuanzisha bendi yake ya African Beat.

**MIKIDADI SEIF**

Alifariki dunia Jumapili Nachingwea mkoani Lindi. Alikuwa mwanamuziki mwimbaji tegemeo wa bendi ya UDA Jazz, wakati huo akitunga vibao vilivyoipaisha sana bendi hiyo kama vile 'Tulele Tuboe', ulioimbwa kwa lugha ya Kimwera, lakini 'Nenda Kaishi Salama' na nyingine nyingi.

Alizikwa siku ya Jumatatu huko Nachingwea.

**JERRY JUMA 'MZEE WA MBEZI'**

Siku ya Jumapili, ilitoka habari ya kufariki kwa mpiga kinanda wa kundi la Tanzania One Theatre 'TOT', Jerry Juma, maarufu kama Mzee wa Mbezi.

Alifariki dunia kwenye Hospitali ya Lugalo jijini Dar es Salaam akikokuwa akitibiwa.

Mwanamuziki huyo aliyekuwa akipiga kinanda kwenye kwaya, muziki wa dansi na taarab, alikuwa pia Mwenyekiti wa Chama cha Wanamuziki wa Taarab nchini Tanzania.

Alizikwa siku ya Jumanne jijini Dar es Salaam.

**JUMANNE KIBONGE**

Ni mmoja wa wanamuziki waliounda bendi ya Nyanyembe Jazz iliyotoa kibao kilichopendwa cha 'Rangi ya Chungwa', lakini alipoihama bendi hiyo, mwanamuziki huyo aliyekuwa akipiga gitaa la 'rhythm', alikwenda kujiunga na bendi ya Tabora Jazz Band zote za mkoani Tabora. Naye alifariki na kuzikwa wiki hii.




# Hart kwa hili unahitaji pongezi

MWIGIZAJI wa Marekabni, Kevin Hart, hatimaye anatarajia kupata mtoto wa pili katika ndoa yake na mkewe Eniko.

Hart ametambulisha ujio wa mtoto huyo ambaye anatarajiwa miezi michache inayokuja.

"Mwanamke mrembo na mke wangu, tunakupenda Eniko Hart, tunajaribu kumpokea mtoto wetu mwingine wa kike na kutufanya tuwe familia ya watu sita," amesema Hart.



## Katy pole yako, corona bado ipo

MWANAMUZIKI nyota wa Pop wa Marekani, Katy Perry, ambaye kwa sasa ni mjamzito, amesema ugonjwa wa corona umemuathiri.

Katika ukurasa wake wa Twitter, Katy, kutokana na kukaa kwa muda mrefu ndani amekuwa na mawazo mengi kiasi cha kumfanya kuwa na msongo wa mawazo.

Amesema, v irusi vya corona vimetikisa sehemu nyingi za ulimwengu kwa njia ambazo hazijafikiriwa na vimesababisha wasiwasi kwa watu.

## Kcee hongera kuongeza familia

MWIMBAJI wa Nigeria, Kingsley Okonkwo, anayejuliakana kama Kcee, na mkewe Ijeoma, wamepata mtoto mwingine wa kiume.

Katika ukurasa wake wa Instagram, mwanamuziki huyo ametambulisha ujio wa mtoto huyo mapema wiki hii na kwenda sambamba na siku ya kuzaliwa mke wake.

"Kama ukitaka kuhesabu siku ya bahati kwangu ni hii, kwanza mke wangu amejifungua mtoto wetu wa kiume na pili imekuwa siku yake ya kuzaliwa," amesema.





## E-Pesa umeyataka mwenyewe

JESHI la Polisi nchini Nigeria, limemwondolea ulinzi mwanamuziki wa Mogul na mfanyabiashara, Emeka Okonkwo, baada ya kudaiwa kutumia vibaya nafasi hiyo.

Inspekta Mkuu wa Polisi, Mohammed Adamu, ameamuru kuondolewa haraka kwa polisi wanaolinda Okonkwo, anayejulikana pia kama E-Pesa, baada ya watu kulalamika anatumia vibaya walinzi hao.

"Ndio naweza kudhibitisha kwamba polisi wameondolewa kumpa ulinzi," amesema.

## Nina wenzio walifanya hivi, ikaishia hewani

Aliyekuwa mshiriki wa shindano la Big Brother Nigeria, Nina Ivy, kwa mara ya kwanza ameweka hadharani pete aliyevishwa na mpenzi wake.

Nina ambaye alishiriki BBNaij 2018, kwa sasa ni mjamzito na pete hiyo inaashiria yupo mbioni kufunga ndoa.

Staa huyo ambaye anaishi Marekani, ameonyesha pete hiyo ya gharama ya madini ya almasi yake kupitia ukurasa wake wa Instagram, huku akiwaacha mashabiki wake wakiwa na maoni tofauti.






Mjumbe wa Bodi ya Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (Tamwa)-Zanzibar, Aziza Juma Ali (kushoto), akimkabidhi baadhi ya vifaa vya kujikinga mwanachama wa Jumuiya ya Habari za Maendeleo Zanzibar, Khatib Sleiman, kwa niaba ya waandishi wengine. Vifaa ambavyo vimetengenezwa na wajasiriamali wanawake. **PICHA: TAMWA ZANZIBAR**

# Wanawake Zanzibar wajinufaisha kiuchumi kupitia Covid-19

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAKATI vita vya kupambana na virusi vya corona ikizidi kushika kasi duniani, hali imekuwa tofauti kwa baadhi ya wafanyabiashara wa visiwani Zanzibar, ambao wanatumia nafasi hiyo kujiinua kiuchumi.

Baadhi ya wajasiriamali hao wameamua kuchangamkia fursa zinazojitokeza katika kukabiliana na corona, kwa kujiingiza katika biashara za kutengeneza na kuuza bidhaa za sabuni, barakoa na vitakasa mikono.

Wakizungumza na mwandishi wa Makala hii, baadhi ya wajasiriamali hao wanasema licha ya ugonjwa huo kuathiri jamii, pia imewafanya kutafuta mbinu za kuongeza mapato yao kwa kuzalisha vitu ambavyo vinaweza kupambana na virusi hivyo vya COVID-19.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO) matumizi ya barakoa, kunawa mikono kwa kutimia maji na sabuni ni njia salama kujikinga na maambukizo ya corona.

Mwanachama wa kikundi cha ujasiriamali cha Wilaya ya Kati Unguja, Zeyana Seif Salum, anasema katika kipindi hiki bidhaa za maji zina soko kubwa kutokana na kuhitajika na watu wengi.

"Corona kwetu imekuwa ni fursa kubwa, kabla ya kuenea kwa ugonjwa huu soko lilikuwa finyu, lakini sasa mahitaji yamekuwa makubwa," anasema.

Zeyana anasema kwamba sabuni wanayozalisha ina ubora unaotakiwa na kabla ya kusambaza sokoni imepimwa na kukubalika na taasisi ya viwango Zanzibar.

**KIPATO**

Hata hivyo, anaeleza kabla ya kuingia kwa corona visiwani humo, walikuwa wanapata shida kupata wateja na mara nyingi walikwenda kuwauzia wafanyakazi katika ofisi za serikali na watu binafsi.

Akitolea mfano, katika kipindi hiki zaidi ya lita 1,300 za sabuni wameziuza na bado wanazalisha nyingine ambayo wateja wanasubiri.

"Kidumu kimoja cha sabuni cha lita tano tunauza kwa Sh. 15,000, wateja wetu wakubwa ni Taasisi ya Milele Fondation na Shirika la Kuhudumia Watoto la Save the Children," anaongeza kusema.

Zawadi Muhamed Abdallah mjasiriamali kutoka Kijiji cha Ukongoroni, anasema kipato kinachotokana na mauzo ya bidhaa zao kimewasaidia kutunza familia zao.

"Soko ni zuri, tunauza sabuni kwa jumla na rejareja kila siku, pesa tunazozipata tunatumia kutunza familia zetu na kulipia mambo mengine muhimu," anasema Zawadi.

Anawapongeza watu waliojitokeza kuwapa mafunzo ya jinsi ya kuzalisha kwa wingi bidhaa hiyo, kulingana na ongezeko la mahitaji ya kila siku.

Sada Muhammed Ali, kutoka Shehia ya Mtende, anasema hakuna anayefurahia kuwapo kwa ugonjwa huo ambao unahatarisha nguvu kazi ya taifa, lakini wao kama wanawake hawakukaa nyumbani, badala yake wanapambana na huku wakijiinua kiuchumi.

**CHANGAMOTO YA UZALISHAJI**

Katika jambo zuri hakukosi changamoto, kwa upande wa wajasiriamali hao wanakabiliwa na tatizo la ukosefu wa vifungashio baada ya uzalishaji kuwa mkubwa.

Sada akawataka viwanda na wafanyabiashara kupeleka kwa wingi vifungashio hivyo kwa ajili ya kuwezesha bidhaa zao kuingizwa sokoni katika muda unaopendekezwa.

Hata hivyo, anasema vifungashio hivyo vichache wanavyopata, wanauziwa kwa bei ya juu, kiasi cha Sh. 12,000, badala ya Sh. 900 ya awali kabla ya ugonjwa wa corona.

Mfanyabiashara anayesambaza ni mmoja pekee ndani ya Zanzibar, anapatikana eneo la Darajani Mjini Unguja, hivyo anawaomba wengine kujitokeza ili kuwe na ushindani wa kibiashara.

"Tunaomba tusogezewe huduma ya vifungashio hadi vijijini, kwa sababu duka lipo moja pekee, wakati mwingine unaambiwa vimemalizaka," anazidi kusema Sada.

**"Kidumu kimoja cha sabuni cha lita tano tunauza kwa Sh. 15,000, wateja wetu wakubwa ni Taasisi ya Milele Fondation na Shirika la Kuhudumia Watoto la Save the Children," anaongeza kusema.**

**KAULI YA TAMWA**

Ofisa mwezeshaji kiuchumi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Tamwa), Mhidini Ramadhan, anasema kuwa corona imetoa fursa kwa wajasiriamali ambao wanajiinua kiuchumi.

Anasema Tamwa imekuwa ikifanya kazi za kuwawezesha wanawake kiuchumi na wamekuwa wakiwapatia elimu ya ujasiriamali ikiwamo utengenezaji sabuni, kilimo cha mboga na utengenezaji wa mikoba ya ukili.

"Wajasiriamali wamepata soko zuri kwa kupata tenda mbalimbali kutoka katika taasisi za umma na binafsi katika mapambano haya ya corona. Kipato hiki kimewasaidia wanajamii maskini hasa maeneo ya vijijini," anasema Ramadhan.

Akizungumzia suala la uhaba wa vifungashio, anasema kuna changamoto kubwa kwa sababu mahitaji ni makubwa ukilinganisha na upatikanaji wake.

Kaimu Mkurugenzi wa Mfuko wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Zanzibar (SMIDA), Shadida Ali Salum, anaeleza kwamba baada ya kuibuka kwa janga la corona, waliamua kukusanya wanawake wajasiriamali na kuwapatia mafunzo ya utengenezaji wa sabuni na vitakasa mikono ili bidhaa hizo ziwapo kwa wingi.

Amewataka wanawake wengine kwenda SMIDA kwa ajili ya kupata mkopo wa fedha kwa ajili ya kununua vifungashio sehemu mbalimbali na kwenda kuwauzia wajasiriamali hao.

"Hivi sasa hatuagizi sabuni za maji kutoka nje ya nchi, tunatumia zinazotengenezwa na wajasiriamali wetu wa hapa Zanzibar, kwa kweli wengi wao wapo vizuri, bidhaa zao ni nzuri," anazidi kusisitiza.

Waziri wa Biashara na Viwanda, Balozi Amina Salum Ali, amewataka wajasiriamali hasa wanawake, kuongeza uzalishaji wa bidhaa ikiwamo sabuni ya maji, vitakasa mikono na barakoa kwani soko lake ni kubwa katika kipindi hiki cha janga la corona.

"Tunataka wajasiriamali wetu waitumie fursa hii katika kipindi hiki kuuza bidhaa zao kwa wingi na kuweza kupata kipato ambacho kitawainua kiuchumi na kuondokana na hali ya utegemezi," anasema Balozi Amina.

Aidha, Balozi Amina, licha ya kukiri ugonjwa wa corona kuteteresha uchumi wa Zanzibar, lakini amefurahishwa kuona wajasiriamali wanawake wanasimama imara kutumia fursa hiyo kupata kipato na kukuza uchumi wao.

## VITA COVID -19

# Vituo watoto yatima kuelimishwa kujikinga

**Na Moshi Lusonzo**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, amewahimiza wananchi kuendelea na mapambano dhidi ya ugonjwa wa COVID -19.

Waziri huyo, kila mara anakaririwa akitahadharisha kwamba, virusi vya corona bado vipo na kila mtu anatakiwa kuchukua hatua za kujilinda kwa kufuata kanuni za afya zilizotolewa na wataalamu.

Njia zinazopendekezwa ni pamoja na kunawa mikono kwa sabuni, kutumia vitakasa mikono kila mara na kuvaa barakoa kila ninapotoka nyumbani.

Hata hivyo, Waziri Ummy, anashauri itumike jitahada kubwa katika utoaji wa elimu kuhusu ugonjwa huo, ili kila Mtanzania afahamu njia za kujikinga nao.

Jumuiya ya vijana inayojulikana kama Nyota Njema, imeamua kutekeleza ushauri huo kwa vitendo, baada ya kuandaa kongamano maalumu litakalozungumzia adhari na athari zitokanazo na corona.

Kongamano hilo litahusisha viongozi na watoto wanaishi katika vituo mbalimbali vya yatima jijini Dar es Salaam, na litaendeshwa kwa kutumia teknolojia ya mtandao, kutokana na serikali kupiga marufuku mikusanyiko ya watu.

Akizungumza na Nipashe, Meneja mradi wa jumuiya hiyo, Ismail Hassan, anasema kongamano hilo litafanyika kesho na kutumia muda wa saa tano.

Washiriki hao na wataalamu wa afya watounganishwa kwa njia ya video wakijifunza mbinu mbalimbali za kukabiliana na corona.

Anasema, Nyota Njema imeona kuna umuhimu wa kujikita katika kundi hilo ambalo anadai lipo hatarini dhidi ya COVD -19.

Hassan, anaeleza kwamba kwa kutumia mtandao wa Zoom, wakuu wa vituo hivyo watapata nafasi ya kujifunza na kuwauliza maswali wataalamu kuhusu madhara na njia ya kujilinda wakiwa kwenye maeneo yao.

“Vituo vya watoto yatima wako nyuma katika mapambano haya ya corona, sisi kama vijana tumeona kuna umuhimu wa kuwapa elimu ili wafahamu namna ugonjwa huu unavyoathiri jamii na namna gani wanaweza kuwakinga watoto,” anasema Hassan.

Katika utoaji wa elimu hiyo, vijana hao watashirikiana na taasisi mbalimbali ikiwamo An Nahl Trust na Islamic Development Agency (IDA).

“Watoto yatima wana haki kama wengine, lengo letu na washirika wetu ni kuona wanafahamu vizuri ugonjwa huu kama wale wanaoishi na wazazi wao,” anaongeza kusema.

Kwa upande wa Ofisa Raslimali Watu, Said Zahran, anasema hatua ya kutoa elimu katika vituo hivyo imechukuliwa baada ya kugundua sehemu hizo zenye idadi kubwa ya watoto, hazina ufahamu wa kutosha juu ya ugonjwa huo.

“Kwa miaka mitatu tunajihusisha na usaidizi wa jamii hii ambayo kimsingi inahitaji ukaribu wetu ili wasijione kama wametengwa. Tangu kuanza matatizo ya corona hakuna jitihada zilizofanyika kuwanusuru na ndio maana sisi tumeona tuanze nao kabla ya kuwafikia wengine,” anasisitiza Zahran.

Pamoja na kongamano hilo, Zahran anaeleza wanaendelea na mkakati wao wa kuwaweka karibu watoto hao, hasa katika mfungo wa mwezi wa Ramadhan unaoendelea.

Katika utekelezaji makakati huo, kituo cha Ally Bin Abutwalib kilichopo Chanika, kimenufaika kwa kupatiwa vyakula mbalimbali.

Kituo hicho kinachohifadhi watoto 55, walipata msaada wa mchele kilo 100, maharagwe kilo 120, ngano kilo 100, mafuta ya kula lita 30, tende pakiti 35 na sabuni miche 100.

“Kila mwaka huwa tunawakaribisha watoto kwa ajili kufuturu pamoja, lakini kutokana na ugonjwa wa corona tumeamua kuwafuata na kuwapa vyakula muhimu ili nao wafurahi na kuona tunawathamini,” anasema Zahran.

Aidha, anasema pamoja na msaada huo, jumuiya hiyo imeguswa na hali duni ya mazingira ya kituo, na imeahidi kutafuta wafadhili ambao wataboresha kwa kujenga uzio.

Naye Farid Mbaraka, ambaye ni Ofisa Uhusiano, anasema utekelezaji wa miradi yote iliyo chini ya jumuiya, inafanywa kwa pamoja kati ya wanachama, taasisi za serikali na watu binafsi.

Anafafanua kwamba, Nyota Njema inafanya kazi ya kuibua matatizo yanayojitokeza katika jamii hasa zile zinazoishi katika mazingira magumu, kisha inakusanya nguvu kutoka sehemu mbalimbali ili kupata ufumbuzi.

“Haya yote tunayafanya kutokana na ushirikiano wetu kama vijana, hatuna pesa za kutosha, lakini uwajibikaji wetu katika kutafuta watu wa kutusaidia tunaweza kuwafikia watu wengi wenye shida na kutatua baadhi ya matatizo,” anasema Mbaraka.



Ofisa Miradi wa Jumuiya ya Nyota Njema, Ismail Hassan, akiwa na watoto wa kituo cha Ally Bin Twalib kilichopo Chanika jijini Dar es Salaam.




Mtoto akipokea msaada wa chakula kutoka kwa kiongozi wa Jumuiya ya Nyota Njema. **PICHA ZOTE: MOSHI LUSONZO**

HABARI KIMATAIFA

# Ofisa afya aonya corona kuangamiza watu

**WASHINGTON,** Marekani

OFISA wa afya wa ngazi za juu wa Marekani, Rick Bright, ameonya nchi hiyo kuwa inaweza kukabiliwa na kipindi kibaya kuwahi kushuhudiwa, kutokana na kasi ya kusambaa kwa maambukizo ya corona.

Bright, ambaye aliongoza shirika la serikali ambalo linajaribu kutengeneza chanjo ya ugonjwa huo, aliondolewa kazini mwezi uliopita baada ya kuelezea hofu yake kuhusu dawa zinazopigiwa debe na Rais Donald Trump.

Akizungumza katika kikao cha wabunge la wawakilishi, Bright, alisema aliondolewa kazini na Rais Trump, kwa madai alikuwa mtumishi asiyeridhika.

**Bila mpango bora, 2020 kunaweza kuwa na kipindi kibaya zaidi cha majira ya baridi kuwahi kushuhudiwa katika historia ya sasa.**

Bright alikiambia kikao hicho kuwa 'maisha ya Wamarekani yanapotea kwa sababu ya serikali kushindwa kuchukua hatua za mwanzo za mlipuko wa virusi vya corona.

Alisema, kuwa kwa mara ya kwanza alizungumzia juu ya ukosefu wa zana za matibabu mwezi Januari, na kufikisha suala hilo katika ngazi za juu za Wizara ya Afya na Huduma za Binadamu (HHS), lakini hakujibiwa.

Wakati akitoa ushahidi huo, alionya kwamba dirisha la kupambana na virusi vya corona linakaribia kufungwa na hakuna njia ya kuokoa.

"Kama tutashindwa kuboresha jinsi tunavyokabiliana na ugonjwa huu kwa misingi ya sayansi, ninaogopa janga litakuwa baya sana na kuendelea kwa muda mrefu," alisema.

"Bila mpango bora, 2020 kunaweza kuwa na kipindi kibaya zaidi cha majira ya baridi kuwahi kushuhudiwa katika historia ya sasa," alionya.

Mtaalamu huyo wa afya aliiambia kamati hiyo kuwa mwezi Januari, alipokea barua pepe ambayo hawezi kuisahau kutoka kwa wasambazaji wa barakoa za hospitali, akionya juu ya upungufu wa vifaa hivyo.

Bright alisisitiza kufukuzwa kwake kazini, kulitokana na kuendelea kwake kusisitiza kuhusu pesa zilizotengwa na 'congresi' za kupambana na mlipuko wa virusi hivyo.

Pesa hizo zililenga kupata suluhu za kisayansi, badala ya dawa, chanjo au teknolojia nyingine ambazo hazijathibitishwa kitaalamu. **BBC**



Raia wa China wakiwa wamevaa barakoa huku wakicheza muziki juu ya daraja la mto Yangtze, mjini Wuhan kabla mamlaka ya Jimbo la Hubei, kuwazuia watu kutoka nje kutokana na maambukizo mapya ya Covid- 19. **PICHA: REUTERS**

## Vifo vya corona vyaongezeka mataifa tajiri

**PARIS,** Ufaransa

MAREKANI inaendelea kuongoza kwa kuwa na visa vingi vya wagonjwa wa corona, huku vifo vikifikia watu 85,194.

Katika rekodi iliyochukuliwa hadi jana, Uingereza inashika nafasi ya pili kwa kuwa na vifo 33,614, Italia ya tatu watu 31,368, Ufaransa 27,425 na Uhispania watu 27,321. Katika orodha hiyo, Brazil imesajiri maambukizo mapya ya virusi vya corona 13,944 na vifo 844.

Rekodi hizo zimetolewa na Wizara za Afya za nchi husika katika kipindi cha saa 24.

Katika hatua nyingine, Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron, atakutana na Mtendaji Mkuu wa kampuni kubwa ya kutengeneza dawa ya Sanofi, Paul Hudson, baada ya siku chache zilizopita mkuu huyo kuikasirisha serikali baada ya kusema baadhi ya mataifa yatapewa kupaumbele katika upatikanaji wa chanjo ya virusi vya corona.

Hata hivyo, Hudson, aliomba radhi kwa kauli yake hiyo na kusema ni muhimu kwa chanjo yoyote ya corona, iwafikie watu wote ulimwengu. **DW**

## Rais Trump atishia kusitisha uhusiano na China

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani, Donald Trump, ametishia kusitisha uhusiano na China kutokana na madai yake kuwa taifa hilo linawajibika kusambaa kwa virusi vya corona duniani.

Katika mahojiano yaliyorushwa jana, Rais Trump amerudia shutuma zake dhidi ya China, akidai ilificha ukweli kuhusu ukubwa wa janga hilo, wakati virusi vilipozuka mjini Wuhan mwishoni mwa mwaka jana.

Akuzungumzia hatua ambazo nchi yake inaweza kuchukua dhidi ya China, Rais Trump amesema taifa lake linaweza kusitisha uhusiano wote uliopo na China.

Marekani imerekodi zaidi ya vifo 86,000 kutokana na virusi vya corona, ambayo ni idadi kubwa kuliko taifa jingine lolote, huku ikiwa na karibu theluthi moja ya maambukizo ya virusi hivyo duniani. **DW**

## Corona yaingia rasmi kambi za Warohingya

**DHAKA,** Bangladesh

WAFANYAKAZI wa afya wanaohudumia wakimbizi wa Kirohingya, wameanza juhudi za kuzuia kusambaa kwa virusi vya corona kwenye kambi wanayohifadhiwa.

Kiasi cha wakimbizi milioni moja ya jamii ya wachache ya waislamu wa Rohingya, wanahifadhiwa katika kambi hiyo nchini Bangladesh.

Kisa cha kwanza cha virusi kimeripotiwa ndani ya kambi na mkazi mwingine wa wilaya ya Cox´s Bazar iliyopo kusini ya Bangladesh amegundulika kuwa na virusi vya corona.

Msemaji wa Shirika la Umoja wa Mataifa la kushughulikia wakimbizi, amesema watoa huduma za afya tayari wameanza kuwahudumia wagonjwa hao wawili, pamoja na kuwafuatilia wote waliokutana nao kwa lengo la kuwaweka karantini.

Kwa muda mrefu kumekuwa na wasiwasi kwamba virusi vya corona vitasambaa kwa kasi iwapo vitaingia katika kambi 34, zinazowahifadhi wakimbizi wa Rohingya kutokana na kuwa na hali mbaya ya miundombinu. **DW**

# HADITHI

ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote, afanye chochote kile ili awenavyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.

Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele. Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo. Hapo ndipo uhai wa Shani unapokuwa matatani na patashika nguo kuchanika inapoanza. Fuatilia mkasa huu kuburudisha, kuelimisha na kusikitisha.

# Mauaji Harusini- 16

Mtunzi anapatikana (0716 350534)




**Na Adam Fungamwango**

Msichana aliinua macho na kumtazama kwa makini Eddy, huku akitazama kidole chake kilipoelekezwa.

Ndipo msichana huyo aliposhtuka, kwani kaburi alilolionyesha jamaa aliyekuwa naye hapo ni la mke wa baba yake, ambao waliuawa pamoja, saa chache tu baada ya harusi.

Alichoona Eddy ni machozi ya msichana huyo kutiririka badala ya jibu. Kama mwanaume alijua jukumu lake.

Alimkumbatia na kuanza kumbembeleza. "Usilie mama, au kuna kitu nimekosea?"

"Kwani we hujui? Kwani we hujui?" Alilia kwa kwikwi mtoto wa watu.

"Sijui. Mimi ninachojua hilo nililokuonyesha ni kaburi la shangazi yangu."

"Hawezi kuwa shangazi yako, wakati hujui nini kilitokea." Msichana alizidi kulia.

"Najua. Ila kuna mengine siwezi kujua kwa sababu sikuwepo nchini."

Jibu hilo lilimfanya msichana huyo anyamaze kidogo na kumwangalia kwa makini mwanaume aliyemkumbatia kimbembeleza wakiwa wawili tu kaburini, majira ya saa nne asubuhi.

**Nikushukuru rafiki yangu Kamal. Kwa muda mfupi tu tumekutana hapa makaburini, lakini umenipa kampani ya kutosha. Mimi narudi nyumbani, naomba namba zako, nitakutafuta siku nyingine ili tuongee zaidi, maana naona kama vile sisi ni ndugu.**

"Ni kwamba, mimi nilikuwa nchini Marekani. Nikiwa huko nilipata taarifa kuwa shangazi yangu ameuawa. Lakini kuuawa kwake aliuawa pamoja na mwanaume mmoja aliyefunga naye ndoa. Mimi huyo mwanaume simjui, sijawahi kumuona, lakini nimeambiwa kuwa waliuawa wakiwa wametoka kufunga ndoa." Eddy alijibu, jibu ambalo kidogo lilionekana kama kumfariji msichana huyo.

"Basi huyu baba yangu ndiye alikuwa mume wa huyo aliyekuwa kwenye kaburi hilo ulilonionyesha." Msichana alijibu na kuanza kulia tena.

"Baba yako ndiyo mume wa shangazi yangu?" Eddy aliuliza.

"Kama ndiyo unayemsema huyo aliyezikwa kwenye kaburi hilo Grace Maumba ni shangazi yako, basi ndiye aliyekuwa mke wa baba yangu mzazi na ndiyo waliouawa wote wakitoka kufunga ndoa." Bado Msichana huyo alikuwa akielezea akilia kwa kwikwi.

"Wewe mwenyewe unaitwa nani?"

"Naitwa Shani."

"Baba yako alikuwa anaitwa nani?"

"Patiyo."

"Nadhani ndiyo alikuwa mume wa shangazi yangu."

Shani aliitikia kwa kichwa.

Joto kali la ujana la msichana Shani liliingia kwenye kifua cha Eddy.

Alikuwa amemwegemea huku machozi yakimtoka.

"Pole Shani, najua jinsi unavyoumia kwa kumkosa baba yako kutokana na baadhi ya watu wenye roho mbaya.

Nakuahidi, watu wote waliofanya mauaji haya, na yeyote aliye nyuma ya mpango huu, ni lazima watapatikana na kulipa maovu yote haya." Eddy aliongea kwa sauti ya chini, lakini yenye mamlaka na msisitizo, ikipenya vema kwenye masikio ya mwanadada Shani.

Msichana alionekana kushtuka kidogo na maneno yale ya kijasiri. Akainua kichwa na kumtazama mtu ambaye maneno hayo yametoka kinywani mwake.

Ni maneno yaliyomtia faraja Shani. Alianza kumuamini mtu yule kwa sababu aliona ana nasaba na marehemu mama yake wa kambo Grace, lakini kwa sasa ni kama aliona si hivyo tu, bali ni mtu ambaye alimhitaji kwa ajili ya kutoa simanzi aliyokuwa nayo.

Bado Shani alikuwa amejiegemeza kwenye kifua cha Eddy.

"Mimi namuachia Mungu tu, atalipa." Ghafla Shani alitoa maneno hayo na kufuatia kilio kikali cha kwikwi.

"Usilie. Msichana mdogo, mzuri na mrembo kama wewe hupaswi kulia hapa. Angalia watu waliopita njiani wanakuangalia unavyolia. Mimi mwenyewe nimeumia kutokana na kifo cha shangazi yangu, lakini silii. Mungu anasema umuombe huku na wewe unafanya kazi. Kazi itakayofuata sasa ni kuwasaka wauaji."

Maneno hayo yaliendelea kumshangaza na kumshtusha Shani. Aliwaza kuwa huenda hakuwa anaongea na mtu wa kawaida "Au mzimu, maana huku ni makaburini?" Alijisemea mwenyewe.

Kwa mbali akaanza kumuogopa. Lakini hakuweza kujiondoa kwenye kifua chake kwa sababu ambazo hata mwenyewe hakuzifahamu.

"Uwasake wauaji, kwani unawajua?"

"Siwajui?"

"Sasa utawasaka vipi?"

Eddy aliachia tabasamu pana la kujiamini. "Hakuna yoyote atakayefanya kitu chochote duniani kwa siri kikakosa kujulikana."

Shani alizidi kupatwa na mshangao juu ya kijana yule aliyekutana naye makaburini. Pamoja na utanashati wake, lakini alionekana ni mtu anayejiamini "Kingine nini vile?" Alijiuliza. Lakini hakupata jibu.

"Kwani wewe unaitwa nani?" Shani kwa mara ya kwanza naye alimuuliza.

"Naitwa Eddy Kamal"

"Ni askari wewe kwani."

"Hapana, mimi nilikwambia mwanzo nimetoka kusoma Marekani. Kwa sasa sina kazi yoyote ile."

"Uko nyumbani tu?"

"Ndiyo maana yake."

Kwa kipindi kifupi tu, Shani alitokea kumuamini na kupenda staili za kijana huyu mwenye tabia ya kujiamini.

"Nadhani sasa tuondoke." Eddy alimwambia.

Kwa shida Shani alijipapatua kwenye kifua cha Eddy na kuanza kutembea taratibu.

Alikuwa akijishangaa awali alikuja akiwa na nguvu, lakini kwa sasa ni kama ameishiwa nguvu, huku akionekana kujidekeza zaidi. "Sababu ni nini?" Alijiuliza. Hakupata jibu.

Hatua chache mbele, gari aina ya Land Cruiser nyeusi ilikuwa imeengeshwa. Na ndipo hatua za Shani zilipokomea.

"Nikushukuru rafiki yangu Kamal. Kwa muda mfupi tu tumekutana hapa makaburini, lakini umenipa kampani ya kutosha. Mimi narudi nyumbani, naomba namba zako, nitakutafuta siku nyingine ili tuongee zaidi, maana naona kama vile sisi ni ndugu." Shani alisema huku akimpa mkono wa kwaheri Eddy.

Wakati huo Shani alikuwa anafungua mlango wa gari hilo. Eddy hakushangaa sana kwa sababu tangu yupo nchini Marekani alisikia kuwa mjomba wake aliyemuoa shangazi yake Patiyo alikuwa tajiri mkubwa.

"Usihofu mtoto wa shangazi yangu, nitajie wewe namba zako, halafu nitapiga ili wewe upate za kwangu na mimi za kwako. Nadhani kila mtu akipata za mwenzake itakuwa vema zaidi.

Shani akafanya kama alivyoambiwa. Baada ya Shani kuondoka, aliliendea gari lake Toyota Revis, naye taratibu akaanza kukata mitaa ya Kinondoni makaburini akirejea kwake Kijitonyama.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KALRAV VINODBHAI PATEL** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 692 DSE TOYOTA RACTIS.

Chassis namba NCP1000020144. Engine namba INZB986218.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya Polisi: DSM/PHQ/RB/379528/2020**

157425

## KUPOTELEWA KWA KADI YA GARI

**Prosper Mmbando** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili T 992 BZJ Chassia No.AT2120013656 na Engine No. 5AB992212.

Yeyote atayeiona atoe taarifa kituo Cha polisi.

Taarifa ya Polisi: **DOD/DOD/RB/341482/2020**

157428

**JAMUHURI WA MUUNGANO WA TANZANIA**
**Mahakama**
**Usimamizi wa mirathi**
**(S.M.M 1984 Nyongeza ya 5 kanuni 2)**
**Katika Mahakama ya mwanzo Dodoma**
**Usimamizi wa mirathi 35/2020**

Ombi la TABITHA FAUSTINE SOBAJA kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi marehemu NICODEMAS JOHN NKOLA

Kwa yeyote anauehusika Tanzania Bara.
Watu wote wanaodai kuwa na mahusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 26/5/2020. Kabla ya mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 13/05/2020.

157427

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo:**
**MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;118/2020**

Ombi la **(1) SONDA EZRA MDENDEMI (2)WENDE EZRA MDENDEMI** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu .
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 26/05/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 12/05/2020.

157430

## KUITWA MAHAKAMANI

Chonya Mayolwa popote alipo Katika Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania unafahamishwa kuwa unatakiwa kuleta utetezi wako wa maandishi kabla ya tarehe 03.06.2020 katika Baraza la ardhi ya Wilaya ya Maswa.

Pia unajulishwa kuwa shauri hii limepangwa kusikilizwa tar 03/06/2020 saa 2:30 asubuhi mbele ya mhe. J .F Kanyerinyeri , Mwenyekiti Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Maswa.

Na endapo utakaidi wito huu na kushindwa kutoa utetezi wa maandishi kwa muda uliopangwa baraza la ardhi wilaya ya Maswa litalazimika kusikiliza shauri hilo upande mmoja na kutoa uamuzi dhidi yako.

1157421

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SGA SECURITY (T) LTD** inatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 705 BQS TOYOTA COROLLA. Chassis namba AE1105286301. Engine namba 5AFE12350.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Control No: 99108125111575.**

157420

## KUPOTEA KWA KADI

**Festus Bwaika Biseko** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye usajili wa namba T874 CJY aina Boxer, chasis namba MD2A18424DWL29777, iliyotolewa na Mamlaka ya mapato Tanzania.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa:

**KAG/BUK/R-B/378778/2020**

157422

## Kupotelewa na kadi ya Pikipiki

JUSTIN CLARENCE MBUMA anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya Bajaji yenye namba za usajili MC 195 BFJ Chasis No. MD2A25BZXGWL22088, engine No.AZZWGL32495 rangi blue.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo Cha polisi.

Taarifa ya polisi: DOM/DOD/TR/372523/2020.

157423

## Kupotelewa na kadi ya Gari

**Meshack Abinel Magenge** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari Aina ya Toyota Land cruzer yenye namba za usajili T 797 BZC. Chasis No. FK619K522059. Engine No. 6D17856009 rangi Silver.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo Cha polisi.

Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/R-B/372928/2020.**

157418

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA MBULU**
**(DONGOBESH)**
**MAOMBI NA. 93/2019**
**GITIYANG GISAQAN ............MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
SIMON MUHALE ...................MJIBU MAOMBI
Mdaiwa SIMON MUHALE popote ulipo.

Fahamu kwamba mleta Maombi GITIYANG GISAQAN ameleta Maombi Na. 93/2019 dhidi yako.

Hivyo basi kama unakusudia kupinga maombi hayo unatakiwa ulete majibu yako na uwepo Barazani wewe binafsi, wakili wako au mwakilishi anayekubalika kisheria, Shauri limepangwa kutajwa tarehe 24/6/2020.

Endapo hautatekeleza hayo shauri litasikilizwa upande mmoja na hukumu kutolewa.

Imetolewa na kutiwa saini na mhuri wa Baraza hili leo tarehe 27/4/2020.

157419

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA MBULU**
**(DONGOBESH)**
**MAOMBI NA. 92/2019**
**GITIYANG GISAQAN ...............MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**EMANUEL SIMON ............... MJIBU MAOMBI**

**Mdaiwa EMANUEL SIMON popote ulipo.**

Fahamu kwamba mleta Maombi GITIYANG GISAQAN ameleta Maombi Na. 92/2019 dhida yako.
Hivyo basi kama unakusudia kupinga maombi haya unatakiwa ulete majibu yako na uwepo Barazani wewe binafsi, wakili wako au mwakilishi anayekubalika kisheria, Shauri limepangwa kutajwa tarehe 24/06/2020.

Endapo hautatekeleza hayo shauri litasikilizwa upande mmoja na hukumu kutolewa.

Imetolewa na kutiwa saini na mhuri wa Baraza hili leo tarehe 27/4/2020.

157419


*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako la Nipashe kila

Nipashe MWANGA WA JAMII



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# LEWANDOWSKI: HAALAND TULIA KWANZA BUNDESLIGA

**MUNICH,** Ujerumani

ROBERT Lewandowski amemshauri nyota wa Borussia Dortmund, Erling Haaland kubakia kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga kwa muda mrefu kabla ya "kuchukua hatua nyingine" wakati huu akihusishwa na Real Madrid.

Haaland mwenye umri wa miaka 19, amejiunga na Dortmund Januari mwaka huu, amefunga mabao 12 katika mechi 11 kwenye mashindano yote akiwa pia amefunga mabao 28 nusu ya msimu wa kwanza, magoli 28 akiwa na Salzburg.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway alikuwa mmoja wa wachezaji anayetajwa zaidi barani Ulaya kwa kuwaniwa na klabu nyingi, na Dortmund wakafanikiwa kupata saini yake mapema mwaka huu.

Licha ya Haaland kusisitiza kwamba akili yake inafikiria zaidi kazi yake dimbani, uvumi umezidi kuendelea ukimhusisha na kuwaniwa na Madrid.

Lakini Lewandowski, anayekipiga klabu ya Bayern Munich, amemshauri kinda huyo kufikiria kukaa kwa muda mrefu kwanza Ujerumani, kabla ya kufikiria kuondoka.

"Ana nafasi nzuri ya kutakiwa na klabu nyingi, lakini bado ana muda," amesema Lewandowski, ambaye wakati anatua Ujerumani Dortmund ndio ilikuwa klabu yake ya kwanza, akiwaambia waandishi wa habari.

"Sitaki kumpa presha yoyote kutokana na kauli yangu, lakini mimi naona bado ana muda wa kutosha kufanya hivyo.

# De Jong atajwa kumrithi Busquets

**AMSTERDAM,** Uholanzi

FRENKIE de Jong anaweza kuwa ameridhishwa na msimu wa kwanza pale Barcelona na ana nafasi kubwa ya kufanikiwa kumrithi gwiji, Sergio Busquets, kwa mujibu wa Ronald de Boer.

Mchezaji wa kimataifa wa Uholanzi, De Jong alikumbana na shutuma katika mechi zake za mwanzo tangu ajiunge na Barca akitokea Ajax kwa ada iliyoripotiwa kuwa euro milioni 75 mwaka jana.

De Boer anaamini raia mwenzake huyo wa Uholanzi ameshazoea maisha ya pale kwenye dimba la Camp Nou, hata hivyo, mchezaji mwenzake wa zamani, Matthijs de Ligt amekuwa na wakati mgumu kule Juventus, akiwalinganisha.

"Watu wanasema hajafikia kiwango alichokuwa akicheza Ajax msimu uliopita au na timu ya taifa," amesema De Boer akiiambia BarcaBlog.

"Lakini sio kila mtu anaweza kusema kwamba wamecheza mechi nyingi na timu imara, hivyo nafikiri anafanya vizuri.

"Unaweza kuona mchezaji kijana kama De Ligt alivyokuwa na wakati mgumu, huku kila mmoja alifikiria kwamba anaweza kucheza mara kwa mara tangu mwanzo.






# 'Martinez ni fowadi aliyekamilika'

**BARCELONA,** Hispania

LIONEL Messi amemwelezea, Lautaro Martinez kuwa ni "fowadi aliyekamilika" huku uvumi ukizidi kukua akihusishwa kuwaniwa na mambingwa wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Barcelona.

Nyota wa Inter Milan, Martinez amekuwa akitajwa anaondoka pale Nerazzurri na kwenda Barca, huku miamba hao wa Hispania wakiripotiwa wanamtaka mchezaji huyo ili kuwa mrithi wa muda mrefu wa mkongwe, Luis Suarez.

Messi awali alimsifia mchezaji mwenzake huyo wa Timu ya Taifa ya Argentina, Martinez, ambaye amefunga mabao 16 katika mechi 31 kwenye mashindano yote msimu huu 2019-20 kabla ya ligi kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Alipoulizwa kuhusu Martinez, nyota wa Barca, Messi aliliambia gazeti la Mundo Deportivo: "Nikiwa mkweli, sijui vizuri kama kulikuwa au kuna majadiiano kwa sasa, sina uhakika.

"Nafikiri tayari nilishasema, kwamba Lautaro ni mshambuliaji wa kuvutia, hasa kwa sababu nafikiri ni fowadi aliyekamilika.

"Ana nguvu, anapiga chenga vizuri, anafunga mabao, anajua namna ya kuulinda mpira...lakini tutaona nini kitatokea kuhusu yeye na wachezaji wengine."

# Barca haiwezi kushinda Uefa – Messi

**BARCELONA,** Hispania

LIONEL Messi amesisitiza Barcelona haiwezi kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya isipokuwa kama wataimarisha kiwango chao, akipingana na kauli ya Kocha Mkuu, Quique Setien.

Barca – ambao walirudi kwenye mazoezi ya mchezaji mmoja mmoja wiki iliyopita, walikuwa wajiandaa na mchezo wa pili wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 dhidi ya Napoli baada ya mashindano kusimamishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Miamba hao wa Hispania walitoka sare ya kufungana 1-1 ugenini na Napoli Februari, huku Messi akidai Barca wanaweza wasishinde ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya – akichambua kauli ya Setien aliyoitoa Aprili.

Messi aliulizwa kuhusu Ligi ya Mabingwa Ulaya ambayo inawezekana kuendelea tena Agosti, na mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or akatoa onyo kwa Barca.

"Sijawahi kuwa na shaka na kikosi tulichonacho kwamba tunaweza kushinda mechi zote zilizobaki, lakini sio kwa kucheza kwa namna tulivyokuwa tunacheza," amesema Messi, ambaye ameshinda mataji manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Barca walikuwa wanaongoza kwa pointi mbili kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu dhidi ya wapinzani wao Real Madrid baada ya mechi 27 za LaLiga kabla msimu haujasimamishwa.





# PULISIC ATOA NENO DORTMUND KWA SANCHO

**LONDON,** England

CHRISTIAN Pulisic amemsifia Jadon Sancho kwa "kazi ya kuvutia" aliyoifanya akiwa na Borussia Dortmund na amesema klabu yake hiyo ya zamani imelipa fadhila kwa kuonyesha imani kwa wachezaji vijana.

Sancho alijiunga na Dortmund kutoka Manchester City mwaka 2017 akiwa na umri wa miaka 17, akiamini kwamba kuhamia kwake klabu ya Bundesliga kungempa nafasi ya kucheza mara kwa mara katika kikosi cha kwanza.

Uamuzi wa mchezaji huyo wa kimataifa wa England umelipa haraka na baada ya miaka mitatu sasa, anachukuliwa kama mmoja wa bidhaa muhimu zaidi duniani, huku akiwaniwa na klabu kadhaa zenye majina makubwa.

Pulisic pia alijitengenezea jina mwenyewe pale kwenye Uwanja wa Signal Iduna Park kabla ya kujiunga na Chelsea kuelekea msimu wa 2019-20 na anafurahia Dortmund wanaendelea kukumbatia kipaji cha kijana huyo.

"Ni moja ya sababu kubwa kwanini nilikuwa na mafanikio makubwa pale wakati nikiwa kijana," amesema akiiambia Sky Sports.

"Nafikiri wanawapa nafasi kubwa wachezaji vijana na ni klabu kubwa na nzuri kwenda pale kujiimarisha.

"Sancho alipewa nafasi, kama ilivyokuwa kwa upande wangu, katika daraja la juu kabisa, na wanakuonyesha njia sahihi kuwa wanakuamini na wanakupa nafasi sawa na wachezaji wote."



# *Conte akunwa na kiwango cha Lampard*

**MILAN,** Italia

ANTONIO Conte amefurahishwa na kiwango cha Frank Lampard katika kipindi chake cha kwanza kuwa kocha wa Chelsea na anaamini mchezaji huyo wa zamani wa kimataifa wa England anaweza kuwa mmoja wa makocha bora duniani.

Lampard alichukua mikoba ya ukocha pale Stamford Bridge baada ya Maurizio Sarri kuelekea Juventus.

Conte aliiongoza Chelsea kwa misimu miwili na kumwachia nafasi Sarri, akishinda taji la Ligi Kuu England msimu wa 2016-17 na lile la FA mwaka mmoja baadaye.

Mashabiki wa nyumbani walikuwa wakitoa shutuma kwa Lampard, lakini wachambuzi wengi wa soka walikuwa wanasifia falsafa yake kwa kuwaamini wachezaji vijana kama Tammy Abraham na Mason Mount na Blues wapo nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu England, kabla ya ligi kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

"Nafikiri Frank anafanya kazi nzuri," amesema Conte, ambaye kwa sasa ni kocha wa Inter Milan akiiambia Sky Sports.

"Hii ni timu yake ya pili baada ya kuwa kocha kule Derby County na kuifundisha timu ya Ligi Kuu sio kazi rahisi.

"Nafikiri ana mbinu na akili, na ana uwezo wa kuwa mmoja wa makocha bora kabisa duniani. Anatakiwa kuendelea kufanya kazi kama anavyofanya na namtakia mafanikio bora kabisa ya baadaye."

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MADRID YAJIPANGA KUMSAJILI HAALAND

## ●●● Yaongeza nguvu kunasa saini ya straika huyo ili kuchukua mikoba ya Jovic ambaye...

**MADRID,** Hispania

REAL Madrid inatajwa itaendelea kufuatilia kwa karibu zaidi maendeleo ya mshambuliaji, Erling Haaland baada ya Ligi ya Ujerumani, Bundesliga kurejea tena kuanzia leo, taarifa zinaeleza.

**Vigogo hao wa Hispania wanaingia sokoni kusaka straika ambaye atakuwa na kiwango kama alivyokuwa Cristiano Ronaldo wakati anaichezea klabu hiyo ya Bernabeu, baada ya Luka Jovic kushindwa kung'ara tangu alipotua majira ya joto yaliyopita.**

Kwa mujibu wa gazeti la Mundo Deportivo la Hispania, Madrid imejipanga kumtupia 'jicho la karibu; straika huyo wa Borussia Dortmund Haaland wakati Bundesliga itakaporejea kuanzia wikendi hii.

Haaland amekuwa mmoja wa wachezaji nyota duniani ambaye ana kiwango cha dunia kutokana na kuonyesha uwezo mzuri kabla ya ligi hazijasimama, tangu alipokuwa akiitumikia Red Bull Salzburg na sasa kwenye kikosi cha Dortmund.

Straika huyo mwenye umri wa miaka 19 amefunga mabao 12 katika mechi 11 alizocheza baada ya kujiunga na Dortmund Januari, mwaka huu.

Madrid inamwona mchezaji huyo nyota wa Timu ya Taifa ya Norway kuwa mmoja wa wachezaji muhimu inaowahitaji katika dirisha la usajili litakalofunguliwa baada ya kukosa mshambuliaji mwenye uwezo mzuri wa kuingia na kufanya mashambulizi.

Vigogo hao wa Hispania wanataka kunasa saini ya Haaland mapema iwezekanavyo lakini wamebaini dirisha la usajili litakalofunguliwa linaweza kuwa na changamoto katika kukamilisha mchakato huo.

Hata hivyo, Dortmund haiko tayari kumuuza mchezaji wake huyo na mazungumzo juu ya usajili huo yameshaanza, lakini yakionekana kuwa magumu kwa sababu ya changamoto ya kuwapo kwa janga la ugonjwa wa corona (COVID -19).

Kama Madrid itashindwa kumsajili straika huyo katika majira ya joto mwaka huu, klabu hiyo ya La Liga inaelezwa itarejea kufanya mchakato mwingine wa kunasa saini ya Haaland mwakani ambapo dau lake la uhamisho la pauni milioni 66 litakuwa limekamilika.

Madrid inahaha kusajili straika mpya baada ya Jovic kushindwa kutimiza malengo ya usajili wake tangu alipokuwa klabuni hapo kwa dau la pauni milioni 62 katika majira ya joto mwaka jana.

Jovic amefunga mabao mawili na kutengeneza pasi nyingi za mwisho za mabao kwenye michezo 24 ya mashindano mbalimbali tangu alipotua Madrid msimu huu.

## ZISIKUPITE

### SILVA KUBAKIA MAN CITY

KIUNGO David Silva (34), ambaye mkataba wake na Manchester City unatarajiwa kumalizika Juni 30, mwaka huu amesema yuko tayari kuitumikia klabu hiyo hadi mwisho wa msimu huu. ***(Times - subscription required)***

### MATONDO ANUKIA UNITED

MANCHESTER United imeanza kumfuatilia winga wa Schalke na Timu ya Taifa ya Wales, Rabbi Matondo (19), ili kumsajili kama itashindwa kunasa saini ya mshambuliaji wa Borussia Dortmund na England, Jadon Sancho, ambaye ana umri wa miaka 20. ***(Manchester Evening News)***

### MERTENS KUBAKIA ITALIA

NYOTA anayewindwa na Chelsea, Dries Mertens anajiandaa kubakia katika klabu yake ya Serie A kama mkataba wake na Napoli utamalizika. Inter Milan inatajwa pia kumwinda mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji mwenye umri wa miaka 33. ***(Mail)***

### HAALAND AFUNDWA

STRAIKA wa Bayern Munich na Timu ya Taifa ya Poland, Robert Lewandowski (31), amemshauri mshambuliaji nyota wa Norway, Erling Braut Haaland (19), anayetakiwa na Manchester United pamoja na Real Madrid kubakia Borussia Dortmund kuendeleza kipaji chake. ***(Metro)***

### COUTINHO HAKIJAELEWEKA

WAKALA wa kiungo wa Timu ya Taifa ya Brazil, Philippe Coutinho, amesema hajafanya mazungumzo na klabu yoyote kuhusiana na usajili wa nyota huyo mali ya Barcelona, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Bayern Munich. ***(Talksport)***

### ADAMS SOKONI RASMI

STRAIKA wa Southampton, Che Adams anajiandaa kuingia sokoni kwa dau la pauni milioni 10 au chini yake ifikapo majira ya joto licha ya Leeds United ilikubali kulipa pauni milioni 19 ili kumnasa nyota huyo raia wa England mapema Januari mwaka huu wakati klabu yake ikiwa haijafikia uamuzi wa kumuuza. ***(Football Insider)***

### GOMES AIGOMEA UNITED

KIUNGO wa Manchester United, Angel Gomes (19), ambaye mkataba wake na klabu hiyo utamalizika katika kipindi cha majira ya joto bado hajasaini mkataba mpya kwa sababu ya wasiwasi wa kukosa namba katika kikosi cha kwanza kutokana na United kujiandaa kusajili mchezaji mpya wa nafasi yake. ***(Manchester Evening News)***

### FOYTH KUTUA LEEDS

MABOSI wa Leeds United wamesema watamsajili beki wa Tottenham Hotspur na Timu ya Taifa ya Argentina, Juan Foyth (22), kama watafanikiwa kupanda daraja, kushiriki Ligi Kuu England msimu ujao. ***(Football Insider)***

### EVERTON YASAKA KIPA

EVERTON inajiandaa kumruhusu golikipa wake Mholanzi Maarten Stekelenburg (37), kuondoka baada ya mkataba wake kumalizika mwishoni mwa msimu huu na kusaka mlinda mlango mpya ambaye atampa changamoto mpya, Jordan Pickford (26). ***(Football Insider)***

### TAGLIAFICO KUITOSA AJAX

BEKI wa kushoto wa Ajax, Nicolas Tagliafico ameweka wazi yuko tayari kuondoka klabuni hapo na kwenda kuitumikia timu nyingine kubwa. Nyota huyo wa Argentina anatajwa kutakiwa na Barcelona. ***(Soccernet)***

HABARI MICHEZO

## Ukata waendelea 'kuitesa' Ndanda

**Na Saada Akida**

MABOSI wa Ndanda FC ya mkoani Mtwara wamesema hali ya kukosa fedha waliyokuwa nayo, ndio imesababisha timu yao 'kusuasua' kwa msimu wa pili mfululizo kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, imeelezwa.

Katibu Mkuu wa Ndanda FC, Seleman Kachele, aliliambia gazeti hili klabu yao haikuwa vema kiuchumi na kwa sababu hiyo ilishindwa kupambana katika mechi mbalimbali za ligi hiyo ya juu nchini.

Kachele alisema viongozi walishindwa kusajili wachezaji waliotarajiwa kuisaidia timu na kutakiwa kutumia 'nguvu zaidi' kila ligi hiyo inapoelekea ukingoni.

Alisema hali hiyo inawalazimu kila msimu kuwa na kikosi kipya kwa sababu ya kushindwa kuwabakisha wachezaji wazuri waliowajenga kwa kusajiliwa na timu nyingine ambazo zinawapatia maslahi bora.

"Hatuna fedha, hivyo mchezaji tunampa mkataba wa mwaka mmoja, ataonyesha kiwango kizuri, lakini muda utakapomalizika atahitaji dau kubwa, hatuwezi kumlipa na hivyo huamua kuondoka zake," alisema Kachele.

Aliongeza nguvu ambayo wanatumia wakati huu ili kuinusuru timu isishuke daraja kama ingetumika wakati wa usajili, hali ingekuwa tofauti na waliyonayo sasa.

Alieleza msimu wa 2016/17 na 2017/18 hawakuwa na 'presha' na timu yao ilifanya vizuri kwa sababu walikuwa na wadhamini waliosaidia shughuli za utawala.

## Mamia wamzika Kampira Tanga

**Na Steven William,** MUHEZA

WADAU wa michezo kutoka sehemu mbalimbali nchini walijitokeza katika mazishi ya aliyekuwa mchezaji wa Coastal Union ya jijini Tanga, Mohammed Kampira, yaliyofanyika katika Kijiji cha Ngomeni, wilayani hapa juzi.



Winga huyo mkongwe wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Kampira (pichani), alifariki dunia Jumatano katika Hospitali ya Bombo, Tanga ambapo alikuwa amelazwa ili kupatiwa matibabu.

Hadi anafariki, nyota huyo wa zamani wa Timu ya Mkoa wa Tanga (Tanga Stars), alikuwa mchambuzi wa soka katika kituo cha radio cha TK FM 88.5 cha jijini hapa.

Katibu Mkuu wa Chama cha Soka Tanga (TRFA), Beatrice Mgaya, alisema marehemu Kampira alikuwa akishirikiana na chama hicho katika masuala mbalimbali ya maendeleo.

"Tumepata msiba, Tanga tumepoteza 'jembe', ila tutaendelea kumkumbuka kwa kuyafanyia kazi mawazo yake," alisema Mgaya.

Selemani Jumanne, Mkazi wa kijiji cha Mkanyageni, alisema wadau wa soka wamepoteza mtu muhimu katika mchezo huo na wataendelea kukumbuka mchango alioutoa enzi za uhai wake.

# RUFANI YA TANZANIA FIFA YAFIKIA PAZURI

**Na Saada Akida**

SHIRIKISHO la Soka Nchini (TFF), limesema rufani ya Tanzania dhidi ya wenzao wa Uganda ambao wanawatuhumu kutumia wachezaji wenye umri mkubwa katika mashindano ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia kwa wasichana wa umri chini ya miaka 17 inaelekea 'mahali pazuri'.

Tanzania inayofundishwa na Kocha Mkuu, Bakari Shime iliondolewa katika mashindano hayo baada ya kukubali kichapo cha mabao 5-0 kwenye mchezo wa marudiano uliochezwa ugenini wakati ilipopata ushindi wa magoli 2-1 hapa nyumbani.

**Akizungumza na Nipashe jana, Katibu Mkuu wa TFF, Wilfred Kidao, alisema rufani yao inaenda vizuri na wanaamini haki itatendeka katika kufanya uamuzi.**

Kidao alisema wamepata taarifa kutoka katika Shirikisho la Soka la Dunia (Fifa), rufani hiyo inaendelea kufanyiwa kazi na itakapokamilika watatumiwa rasmi uamuzi uliochukuliwa kwa kupitia ushahidi wote uliowasilishwa na pande hizo mbili.

"Ni mapema kuzungumza kuhusu rufani hiyo, kwa sababu suala hilo lipo katika mikono ya sheria, tunachotakiwa ni kusubiria majibu tutakayopewa, na sisi tutawajulisha wadau wetu tutakachoambiwa," alisema Kidao.

Tanzania ilikata rufani ikipinga Uganda ilitumia wachezaji watano wenye umri mkubwa ambao ni pamoja na Namusisi Joan, Fauzia Najjemba, Nalugya Shamira na nahodha wa timu hiyo Julieth Nalukenge.

Hata hivyo Tanzania bado iko katika kinyang'anyiro cha kusaka tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Dunia kwa wanawake wa umri chini ya miaka 20 baada ya kuwaondoa wenzao wa Burundi. Machi 20, mwaka huu Tanzania ilitarajiwa kuwavaa Senegal, lakini mchezo huo uliahirishwa kutokana na kuwapo kwa janga la corona na hivyo, utapangiwa siku nyingine.



Wachezaji wa Manchester United, Paul Pogba (kulia), na Andreas Pereira wakifanya mazoezi kwenye uwanja wa kriketi wa Cheshire kwa ajili ya kujiandaa na mechi za Ligi Kuu England inayotarajiwa kurejea kuanzia Juni 12, mwaka huu. **PICHA: MAIL**

## *Polisi yalalamika kukosa mastraika*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Msaidizi wa Polisi, Yusuph Ramadhani Sape, amesema kikosi chake kinahitaji kupata washambuliaji bora ili kiweze kufanya vema katika Ligi Kuu Zanzibar ambayo imekuwa na ushindani zaidi msimu huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Sape alisema kikosi hicho hakina washambuliaji wenye uzoefu ambao wanaweza kukabiliana na ushindani na kasi iliyoko katika ligi hiyo ya juu Zanzibar.

Sane alisema changamoto hiyo inazikabili timu mbalimbali za Zanzibar na anawashauri makocha kuandaa programu maalumu ya kuwajenga washambuliaji wapya ili kukisaidia kisiwa hicho.

"Tatizo hili halipo kwa Polisi pekee, ni vema makocha tukaliangalia hili, na hata kuanza kujipanga kutengeneza wachezaji wengine wa nafasi hiyo ili waweze kuzisaidia timu zao na kuleta ushindani," alisema Sane.

Kocha huyo alisema katika maandalizi ya msimu ujao, atapendekeza viongozi wa klabu hiyo kusajili washambuliaji wenye uwezo wa kufunga na hapo watamaliza changamoto hiyo waliyonayo msimu huu.

"Hali hii inatufanya tunashindwa kupachika magoli mengi uwanjani, na muda mwingine tunafungwa, kuelekea msimu ujao, usajili wetu utalitazama kwa jicho kubwa nafasi hii ya ushambuliaji," Sane alisema.

Aliongeza anapambana kuwarejesha wachezaji wake katika ushindani baada ya kukata tamaa na kuamini timu yao itashuka daraja, jambo ambalo wanaweza kuliepuka kama watafanya vizuri kwenye mechi zilizosalia.

Polisi yenye pointi 23 baada ya kushuka dimbani mara 20 iko katika nafasi ya 12 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar.

# Michezo

Jumamosi Mei 16, 2020

Nipashe




Madrid yajipanga kumsajili Haaland UKURASA 22




Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia, ambaye mwaka jana alikuwa mwenyeji wa fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa vijana wa umri chini ya miaka 17 (AFCON U-17). **PICHA: MAKTABA**

## Yanga kigugumizi kwa Mwamnyeto

**Na Saada Akida**

WAKATI dau analolitaka beki wa Coastal Union, Bakari Mwamnyeto, likionekana kuwa na changamoto, uongozi wa Yanga umesema safu yao ya ulinzi inaweza kuendelea kuwa imara bila ya kumsajili nyota huyo wa Timu ya Taifa (Taifa Stars).

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela, alisema safu yao ya ulinzi inamtegemea zaidi, Kelvin Yondani na uwepo wake katika kikosi hicho unawafanya wawe salama.

Mwakalebela alisema wanashangaa kusikia taarifa za kumwania beki huyo ambaye bado ana mkataba na klabu yake.

"Sio kweli hatuwezi kuzungumza na mchezaji mwenye mkataba, taarifa hiyo kwetu ni mpya kabisa, bado hatujafikiria, nafasi anayocheza Mwamnyeto kwa hapa kwetu wapo na wamefanya vizuri, hivyo hatuwezi kumchukua mtu na kumweka benchi," alisema Mwakalebela.

Aliongeza bado hawajafikiria suala la kumsajili beki huyo licha ya kuonyesha kiwango kizuri na kwa sasa wanaendelea kukamilisha mazungumzo na wachezaji wao wanaowahitaji ambao wamemaliza mikataba.

"Bado tunajadiliana na wachezaji wetu waliomaliza mikataba, hatuna mpango na nyota wapya hadi hapo ligi itakapomalizika hasa kwa wale ambao anawahitaji kocha," Mwakalebela alisema.

Taarifa kutoka katika Kamati ya Utendaji ya Coastal Union zinasema thamani ya beki huyo, ni Sh. milioni 100.

Chanzo hicho kinasema kuwa katika fedha hizo, Mwamnyeto atachukua Sh. milioni 80 na kiasi kilichobakia kitakwenda kwa klabu yake na Yanga inakwama kukamilisha mchakato huo kwa sababu imeweka mezani Sh. milioni 80.

Beki huyo aliwahi kuiambia Nipashe anajipanga kuleta mapinduzi katika usajili wa wachezaji wazawa kwa kutokubali kupokea dau chini ya Sh. milioni 100.

# TFF matatani fedha za JPM

## Mabosi wake waanza kuhojiwa, Kidao aitaja Kamati ya Mwakyembe na Tenga ndiyo...

**Na Enock Charles**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), imesema inajiandaa kuwahoji viongozi wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), matumizi ya Sh. bilioni moja zilizotolewa na Rais John Pombe Magufuli hapo mwaka jana, imeelezwa.

**Rais Magufuli alitoa fedha hizo kwa ajili ya maandalizi ya mashindano ya Kombe la Mataifa Afrika kwa vijana wa umri chini ya miaka 17 (AFCON U-17), yaliyokuwa yanafanyika nchini Aprili, mwaka jana.**

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mkuu wa Takukuru, Brigedia John Mbungo, alisema taasisi hiyo inawafanyia uchunguzi viongozi wa TFF katika kuhakikisha waliotumia fedha hizo vibaya wanachukuliwa hatua.

Mbungo alisema fedha hizo zilizotolewa na Rais Magufuli pamoja na michango mingine iliyotolewa na wadau ili kufanikisha mashindano hayo.

"Zile pesa zimetumika vibaya, taasisi inayo taarifa, imechukua ya kufanya uchunguzi, tunawaita watu wote wanaohusika, tunawahoji, tunaendelea kukusanya nyaraka mbalimbali, uchunguzi unaendelea, upo, hawa watu wana hiari ya kuanza kurejesha hizo fedha, uchunguzi upo na unafanyika," alisema Mbungo.

Aliongeza uchunguzi huo unaendelea vizuri na tayari imeshawaita na itawaita wahusika kuwahoji namna ya fedha hizo zilivyotumika.

Mkurugenzi huyo alisema tayari taasisi hiyo imeshawaita wote wanaohusika na sakata hilo kuwahoji na wanaendelea kukusanya nyaraka zinaonyesha ukusanyaji wa fedha hiyo na matumizi yake.

Amewataka wadau wa tasnia ya michezo kutoa taarifa katika mamlaka hiyo pale wanapoona viashiria vya rushwa ili kuiwezesha taasisi yake kufanya uchunguzi kwa haraka na kupata ufumbuzi.

"Bahati mbaya sana watu waliopo kwenye tasnia ya michezo ni wazuri sana kwenye kuongea, ni wazuri sana kwenye kuchambua, ni wazuri sana kwenye kutengeneza dhana na 'hypothesis' nyingi," alisema Mbungo.

"Lakini kitu kimoja ambacho kinatusikitisha pale yanapotokea matatizo ya refa kula rushwa au wachezaji kupokea rushwa hawawi mstari wa mbele kutuletea taarifa," aliongeza.

Katibu Mkuu wa TFF, Wilfred Kidao, aliliambia gazeti hili jana, shirikisho hilo litatoa taarifa rasmi kuhusiana na sakata hilo.

Kidao alisema mchango huo uliotolewa na Rais Magufuli ulikuwa mkubwa kwa kufanikisha mashindano hayo ya AFCON U-17, lakini TFF haikupokea fedha taslimu.

"Hatukupokea hata senti tano," Kidao alisema kwa kifupi.

Hata hivyo katika mahojiano maalum yaliyorushwa mubashara na shirikisho hilo juzi, Kidao alisema fedha hizo zilikuwa chini ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano ya ndani ambaye alikuwa Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe na makamu wake, Mwenyekiti wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Leodegar Tenga.

"Fedha kupokelewa na matumizi yake, yalikuwa yanasimamiwa na vyombo ambavyo vinavyohusika na wizara yenye dhamana ya michezo, sisi kama TFF, fedha hatukupata kupitia kwetu, zilipitia katika mamlaka nyingine ili kufanikisha mashindano yanayofanyika," Kidao alisema juzi.

Alisema TFF ilifaidika na fedha hizo ili kufanikisha mashindano hayo na kulikuwa na chombo kilichoratibu ambacho fedha hizo zilikuwa zinapitia.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >